
DVV International

Education for Everyone. Worldwide
Lifelong.

# Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (MKMEUWAWA)

## Seti ya Zana za Utekelezaji

# Utangulizi wa Mkabala na Seti ya Zana




With financial surpport from the

Federal Ministry
for Economic Cooperation
and Development

**Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (MKMEUWAWA)**

**Seti ya Zana za Utekelezaji**

**Kimechapishwa na:**

Institut für Internationale Zusammenarbeit
des Deutschen Volkshochschul-Verbandes e. V.
(DVV International)

Königswinterer Straße 552b
53227 Bonn

Federal Republic of Germany

Simu. +49 (0) 228-97569-0

Nukushi. +49 (0) 228-97569-55

info@dvv-international.de

www.dvv-international.de

© DVV International 2020

(Toleo la Kwanza)

**Mwandishi & Mbunifu/Mwendeleza Mkabala:**
Sonja Belete

**Mwajibikaji/Mhariri Mtendaji:**
Uwe Gartenschlaeger

**Wasaidizi wa Utafiti:**
Penny Ward (Mutengo Consulting),
Prof. Heribert Hinzen

**Uhakiki/Uhariri wa Kiingereza:**
Penny Ward (Mutengo Consulting)

**Michoro:**
Zerihun Gebrewold Lemma

**Upangaji/Usanifu:**
Gastdesign.de

# Yaliyomo


Shururani....04

Dibaji....05

Vifupisho....06

**UTANGULIZI WA MKABALA NA SETI YA ZANA**....07

**1. Utangulizi**....08

**2. Usuli na Madhumuni**....10

**3. Mchakato na Mbinu za Kuendeleza Mkabala Huu**....12

**4. Kanuni za Msingi na Mazingatio**....13

**5. Viashirio Kuhusu Nadharia na Ulinganishi**....15

**6. Dhana za MKMEUWAWA, Muktadha na Majukumu ya Wadau**....19

6.1 Kuelewa dhana....19

6.2 Kutoa fasili ya kimuktadha na wigo wa kutumia mkabala....21

6.3 Wadau na watekeleza wajibu....21

**7. Kiunzi Dhana cha MKMEUWAWA na Awamu Zake**....23

7.1 Kiunzi dhana cha MKMEUWAWA....23

7.2 Awamu za utekelezaji wa mkabala....29

**8. Mwongozo wa Kutumia Seti ya Zana**....31

8.1 Muundo wa Seti ya Zana....31

8.2 Kabla ya kutumia mkabala na Seti ya Zana....32

Faharasa....33

Marejeleo....34

# Shukurani



Uchapishaji wa seti ya zana hii na mfululizo kuandaa vitabu hivi, usingeweza kukamilika bila ya ushiriki wa karibu wa wafanyakazi wa Shirika la Kimataifa la DVV katika ofisi za nchini Ethiopia na Uganda. na Uganda. Walitumia muda wao mwingi kusoma, kujadili, kupima, kutafakari na kutoa maoni na mawazo mpaka kile kilichoanza kama mfululizo wa warsha kadhaa kiliibua mkabala madhubuti unaotoa mwelekeo wa kazi za DVV kimataifa katika Ukanda wa Mashariki/ Pembe ya Afrika na zaidi ya mipaka hiyo. Mwandishi anatoa shukurani kwa Eshetu Abate, Amanuel Hedera na Caesar Kyebakola.

Washirika wa Shirika la Kimataifa la DVV katika kanda, yaani Wizara ya Elimu (WyE) nchini Ethiopia na Wizara ya Jinsia, Kazi na Maendeleo ya Jamii (WJKMJ) nchini Uganda, wamekuwa mstari wa mbele katika kuthamini uwezo mkubwa wa mkabala huu hata katika hatua zake za awali. Wakishirikiana na wenzao katika ngazi ya serikali za mitaa na ofisi zingine ambazo zilishiriki warsha za mafunzo na tafakuri. Walifanya upitiaji taalimu, walichangia mawazo, na kuzijaribu Seti ya Zana, nadharia pamoja na awamu za mkabala huu. Wanaendelea kuutumia mkabala huu katika kazi zao za kila siku ili kujenga mifumo bora ya EUWAWA.

Shukurani za pekee ziende kwa timu mbili zilizofanya upitiaji ya taalimu kuhusu Mfumo wa Mafunzo na Elimu ya Watu Wazima nchini Ethiopia katika ngazi zote za utekelezaji. Rejea maalumu inafanywa kwa:

- Timu iliyofanya tathmini kwa upande wa utoaji huduma wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (EUWAWA) na utoaji wa huduma ya EUWAWA mwaka 2018. Timu hii ya upitiaji taalimu haikutoa tu taarifa nyingi za msingi kuhusu mfumo huu nchini Ethiopia, bali pia kuzifanyia majaribio zana za Awamu ya Pili katika Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (MKMEUWAWA).
- Timu iliyofanya tathmini kwa upande wa wapokea huduma kuhusu mahitaji na maslahi ya wanafunzi wa EUWAWA kwa mwaka 2019/2020. Matokeo ya utafiti yalitoa msingi wa uchambuzi zaidi wa Awamu ya Pili na kusaidia uandaaji wa Awamu ya Tatu.
- Wafanyakazi wa makao makuu ya Shirika la Kimataifa la DVV waliona umuhimu wa mkabala huu na kuwekeza muda wao mwingi katika kusoma na kutoa maoni yao. Bila msaada wao na kutoa kipaumbele katika kuboresha kazi hii, uandaaji wa Seti ya Zana hii usingekamilika. Neno la shukurani linaelekezwa kwa wafuatao:

- Naibu Mkurugenzi, Uwe Gartenschlager, ambaye alisimamia maandalizi ya Seti ya Zana hii na kutoa mwongozo, mchango, maoni na muda mwingi katika mchakato mzima. Msaada wake ulikuwa wa thamani sana.
- Mkurugenzi Mtendaji, Christoph Jost, kwa kutoa fursa ya kuandaa na kuchapisha Seti ya Zana hii.
- Frauke Heinze, Gerhard Quincke na Esther Hirsch kwa kuwa tayari kupokea na kuendeleza mkabala huu.
- Wafanyakazi wote wa Shirika la Kimataifa la DVV katika Kanda ya Afrika kwa kuthibitisha na kuujaribu mfumo wa dhana, awamu na zana za MKMEUWAWA.

Zaidi ya hayo, ningapenda kuwashukuru washiriki wote, yaani Prof. Heribert Hinzen, kwa msaada wa kiutafiti na mchango kuhusu misingi ya kinadharia ya mkabala huu; Penny Ward kwa kufafanua zana ili kuwezesha michakato na uhariri wa lugha ya Kiingereza (kwa aili ya toleo la Kiingereza); Zerihun Gebrewold aliyeboresha kwa kupunguza maandishi kwa vielelezo vya rangi; Houssem Bel Hadj kwa tafsiri ya Kifaransa na GASTDESIDN kwa mpangilio na usanifu wa picha, na wafasiri wote katika lugha zilizosalia; kazi yenu bora ya kitaalamu sana ilisaidia maandalizi ya nyenzo hii na kuifanya kuwa halisi.

Sonja Belete



Wakati Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipopitisha Malengo ya Maendeleo Endelevu mwaka 2015, kilikuwa ni kipindi cha shangwe katika sekta ya elimu. Kwa mara ya kwanza Jumuiya ya Kimataifa ilikiri kwamba, kujifunza hakuna kikomo, na fursa za kutosha za kujifunza zinapaswa kutolewa kwa watu wa rika, jinsi, jamii na makabila yote. Maendeleo haya yameleta matumaini kwamba wafanya uamuzi wa wadau wakubwa watapanua sera za elimu na kuweka msisitizo mkubwa katika Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (EUWAWA). Hata hivyo, japo ni dhahiri kwamba maboresho kadhaa yamefanyika, EUWAWA ndiyo sekta ndogo iliyopuuzwa zaidi katika mifumo mingi ya elimu kitaifa.

Changamoto kubwa ambayo taasisi nyingi za serikali na zisizo za serikali za elimu ya watu wazima zinakumbana nayo ni ukosefu wa mfumo wa kuendeleza, kufadhili, kufuatilia na kusaidia ujifunzaji wa elimu ya watu wazima (EUWAWA) katika ngazi ya taifa, kanda na ngazi za chini. Wakati nchi nyingi zikiwa na mifumo thabiti kwa ajili ya shule za msingi, sekondari, elimu ya juu na wakati mwingine elimu ya ufundi stadi, hali ni tofauti kwa upande wa EUWAWA.

Shirika la Kimataifa la DVV lina uzoefu wa zaidi ya miaka 50 katika kusaidia uanzishwaji na uboreshaji wa mifumo ya EUWAWA. Tulichojifunza katika jitihada hizi ni kwamba, kufanya kazi bila ushirikiano kuna hatari kubwa ya kushindwa. Pia ndivyo ilivyo kwa michakato ambayo inategemea zaidi utaalamu wa kigeni na mifumo ya kuiga.

Kwa kuzingatia utangulizi huu, timu ya kimataifa ya DVV ya Mashariki/Pembe ya Afrika chini ya uongozi wa Sonja Belete, ilianza mchakato wa kutengeneza modeli kamili ya uboreshaji endelevu wa mifumo ya EUWAWA. Vijitabu hivi vinawasilisha mbinu na uzoefu ambao umeandaliwa kwa muda mrefu. Tuliuita “Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (MKMEUWAWA)” na umejikita katika misingi anuwai ya ukweli:

- jenzi wa mfumo endelevu unatumia muda mwingi, mchakato wa muda mrefu ambao unahitaji uvumilivu na unyumbufu mkubwa.
- Umiliki ndiyo nguzo ya msingi. Wadau wa ndani wanapaswa kuunda mchakato na kutengeneza mfumo. Utaalamu wa nje unaweza kuwa na manufaa lakini haupaswi kuongoza mchakato au kulazimisha masuluhisho.
- Ujenzi wa mfumo unahitaji ujenzi wa makubaliano kati ya washirika muhimu. Kigezo hiki ni muhimu kwa mafanikio; hivyo kinapaswa kuwekwa tangu mwanzo na kiendelee kutumika katika mchakato wote.

Sonja Belete na wenzake walibuni MKMEUWAWA kwa utaratibu wa kuanzia chini kwenda juu (bottom-up manner) hasa kutokana na uzoefu wa nchi za Ethiopia na Uganda. Wakati huohuo, mkabala huo pia umetumiwa na nchi nyingine kumi barani Afrika.

Mchakato huo umeboreshwa kwa kuzingatia kanuni za kujifunza kwa vitendo ili kuhakikisha kwamba miundo na zana zimeandaliwa na kuboreshwa zaidi katika mchakato huu. Kujifunza kwa vitendo ni kigezo muhimu cha mafanikio ya mkabala huu na kinapaswa kutumika wakati wa utekelezaji wa mchakato.

MKMEUWAWA ni mkabala ambao unaweza kuwaongoza wadau katika kazi ngumu ya kujenga mifumo na wakati huohuo unaruhusu maboresho, ulinganisho na mabadiliko!
Tunakutakia mafanikio makubwa katika kujenga na kuboresha mifumo ya Ujifunzaji wa Elimu ya Watu Wazima na tunamatumaini kwamba uzoefu wetu unaweza kuchangia katika kuboresha kazi yenu!

Uwe Gartenschlaeger.

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| **AZISE** | Asasi Zisizo za Serikali |
| **DVV** | Deutscher Volkshochschul-Verband |
| **EMAU** | Elimu na Mafunzo ya Ufundi |
| **EUWAWA** | Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima |
| **KJK** | Kituo cha Jamii cha Kujifunzia |
| **KKK** | Kusoma, Kuandika na Kuhesabu |
| **MD** | Mtaala wa Dunia |
| **MKMEUWAWA** | Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima |
| **MT** | Mtaala wa Taasisi |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TEWW** | Taasisi za Elimu ya Watu Wazima |
| **VEWW** | Vituo vya Elimu ya Watu Wazima |
| **vhs** | Volkshochschulen/shule za sekondari za juu |
| **WJKMJ** | Wizara ya Jinsia, Kazi na Maendeleo ya Jamii |
| **WyE** | Wizara ya Elimu |

# UTANGULIZI WA MKABALA NA SETI YA ZANA

# 1. UTANGULIZI




***"Labda tuingilie kati, hatutaweza kujifunza baadhi ya mienendo muhimu ya mfumo ikoje hasa."***

Kurt Lewin alivyonukuliwa na Schein (Schein, Vol, Number 1)

**Jukumu muhimu la Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (EUWAWA) katika maendeleo ya jamii na kupunguza umaskini, limetambuliwa kwa muda mrefu. Hakuna shaka kwamba EUWAWA ni jambo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii, zaidi ya kuwa haki ya kibinadamu. Inaweza kusaidia kukuza ushiriki hai wa raia katika mambo mbalimbali, kuimarisha ukuaji wa mtu binafsi na kulinda ushirikishwaji wa kijamii na hivyo, kwenda mbali zaidi na kupata ujuzi wa kuajiriwa. Elimu na Ujifunzajji wa Watu Wazima ni sehemu ya mzunguko wa kujifunza kwa maisha yote na ni sekta tofauti ya elimu. Ni zaidi ya ujuzi wa watu wazima kusoma na kuandika na inajumuisha fursa anuwai za kujifunza kwa watu wazima ikiwa ni pamoja na mafunzo nje ya mfumo rasmi, mafunzo ya ujuzi wa biashara, mafunzo ya ujuzi wa maisha na kadhalika. Uchangamani wa sekta hii ya elimu unapaswa kutupa changamoto ya sisi kuingiliana vizuri zaidi na vipengele hivi na kuviimarisha kwa ukweli thabiti (Süssmuth, 2009).**

Shirika la Kimataifa la DVV kama shirika linaloongoza kitaaluma katika nyanja ya elimu ya watu wazima na ushirikiano wa maendeleo, limejizatiti kusaidia elimu endelevu kwa zaidi ya miaka 50. Kama shirika linalofanya kazi duniani kote la EUWAWA, DVV kimataifa, serikali na washirika wa mashirika ya kiraia, inalenga kujenga mifumo endelevu ya elimu ya watu wazima ili kufikia utoaji wa huduma bora katika elimu ya vijana na watu wazima. Hili linahitaji mkabala wa kijumla unaozingatia mfumo wa elimu ya watu wazima kwa ujumla pamoja na vipengele vyake vyote. Katika muktadha huu, Shirika la Kimataifa la DVV limetengeneza Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (MKMEUWAWA) kwa muda wa miaka sita kupitia mchakato wa kujifunza kwa vitendo nchini Ethiopia na Uganda.

Kwa kutumia zana na michakato kutoka elimu ya watu wazima, nadharia ya mifumo, uboreshaji wa utoaji huduma, utawala, usimamizi wa masuala ya umma, maendeleo ya ushirika, na mbinu kadhaa shirikishi, kama vile Mbinu ya Kisomo ya Freire ya Kuwezesha Jamii Kujikomboa (REFLECT), mbinu hii ya Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima ilikuwa kikaboni kwa kupima zana na michakato kwa muda na washirika wa serikali. Kadiri eneo la Mashariki/Pembe ya Afrika lilivyoanza kufanya majaribio kwa Vituo vya Jamii vya Kujifunzia (VJK), kama mahali ambapo huduma mbalimbali za elimu ya watu wazima zingeweza kutolewa, uzoefu huu wa kiutendaji uliingizwa katika maendeleo ya MKMEUWAWA.

Mkabala wa Ujengaji wa Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (MKMEUWAWA) unalenga kuhakikisha kuwa aina mbalimbali za huduma za elimu na elimu ya watu wazima zinatolewa kwa vijana na watu wazima kupitia njia zinazofaa na zinazoweza kufikiwa na ubora unaohitajika wa programu. MKMEUWAWA unatambua kwamba ili kuimarisha utoaji huduma ni muhimu kuchambua vipimo na mchakato halisi wa utoaji na mfumo mzima wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima. Aidha, mfumo huu unabainisha sifa kuu za mfumo na unachunguza urekebishaji upya, upangaji wa michakato ya biashara na mbinu zingine ili kushughulikia changamoto kwa ujumla wake. Kujaribu kushughulikia vyanzo vya changamoto badala ya kushughulika na dalili au matokeo ya changamoto.

# 1. UTANGULIZI

Kiunzi cha dhana ya Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima kinaweka mfumo katika vipengele vinne vikuu ambavyo vimegawanywa zaidi katika vijenzi vya mfumo. Vipengele na mahitaji wezeshi vimeunganishwa na hutegemeana na mianya ya maoni. Mfumo wa dhana unakubali kwamba mawanda ya mifumo ya elimu na ujifunzaji wa watu wazima ina asili jumuishi ambayo inazingatia huduma kama vile kisomo chenye manufaa, pamoja na stadi za ujuzi nje ya mfumo usio rasmi n.k., yaani 'uchangamani mlalo'. Huduma hizi zilizochangamana zinaeleweka na hutolewa katika nyanja zote za utawala (ngazi za juu-kati-chini) 'uchangamani wima', humaanisha kuwa viunganishi na mianya ya maoni vipo kati ya kila nyanja/ngazi ya utekelezaji.

Mtazamo huu unajumuisha awamu tano ambazo zinaweza kusaidia serikali, mashirika ya kiraia na wahusika wengine:

- **Kujenga maafikiano** na wadau wote wa mfumo wa elimu ya watu wazima katika nchi fulani na kufafanua wigo wa mfumo unaohitaji kuboreshwa (Awamu ya Kwanza - Ujenzi wa Maafikiano).
- **Kutathmini hali ya mfumo** katika muktadha wa miradi na programu ambazo ni sehemu ya mfumo wa elimu na elimu ya watu wazima nchini, kubainisha ni vipengele vipi na vizuizi vya ujenzi vya mfumo vilivyopo na jinsi vinavyofanya kazi vizuri (Awamu ya Pili - Sehemu ya Kwanza: Tathmini).
- **Kutathmini zaidi sababu za msingi za vizuizi vya mfumo** kupitia tafiti za uchunguzi (Awamu ya Pili - Sehemu ya Pili: Utambuzi).
- **Kutafuta namna nzuri zaidi ya kuanza ili kushughulikia changamoto** za mfumo kupitia uchanganuzi mbadala na kubuni mfumo mpya (Awamu ya Tatu - Uchambuzi wa Mibadala na Usanifu).
- **Kutekeleza na kuujaribu mfumo mpya ulioundwa** katika maeneo yaliyochaguliwa baada ya muda (Awamu ya Nne - Utekelezaji na Upimaji).
- **Kukagua mfumo uliojaribiwa,** kufanya marekebisho yanayohitajika na kupanua wigo wa kuboresha utoaji wa huduma za elimu ya watu wazima. (Awamu ya Tano - Pitia, Rekebisha na Panua Wigo).

Zana ya Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (MKMEUWAWA) inakusudia kuwasaidia watumiaji wake:

- Kufahamu zaidi Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima na mfumo wake wa dhana, awamu, vipengele na vizuizi vya ujenzi vya mfumo.
- Kubainisha wajibu wao kama wadau na watambue ni eneo gani mahususi la mfumo wa EUWAWA wangependa kushughulikia katika nchi zao.
- Kuchunguza na kutumia mbinu na zana katika kila awamu na kuziweka katika muktadha.
- Kuchangia katika kujenga mfumo ulioboreshwa wa utoaji huduma wa EUWAWA.

Hivi sasa, Seti ya Zana hutoa taarifa za kina zaidi juu ya Awamu ya Kwanza na ya Pili ya mbinu hiyo kwa kuwa Awamu ya Tatu, Nne na Tano bado zinajaribiwa kwa kujifunza kwa vitendo katika eneo la Mashariki na pembe ya Afrika. Hata hivyo, mfumo na zana zilizochaguliwa kwa awamu tatu zilizopita zimejumuishwa kwenye kisanduku cha zana. Kwa kuzingatia kwamba ujenzi wa mfumo wa EUWAWA unaweza kuchukua miaka mingi kukamilika, Seti ya Zana itasasishwa mara tu zana katika awamu tatu zilizopita zitakapotumika na kujaribiwa.

Seti ya Zana ina msururu wa vijitabu vinavyosababisha mtumiaji kupitia mbinu kulingana na awamu tofauti za utekelezaji. Kijitabu cha kwanza kinajumuisha Utangulizi wa Mkabala na Seti za Zana. Ni sehemu muhimu ya kuanzia kwa vijitabu vilivyosalia ambavyo vimepangwa kulingana na awamu za mkabala. Vijitabu vifuatavyo vinapatikana kwenye Seti ya Zana:

- Utangulizi wa Mkabala na Seti za Zana
- Awamu ya Kwanza - Ujenzi wa Makubaliano
- Awamu ya Pili - Tathmini na Utambuzi
- Awamu ya Tatu - Uchambuzi wa Mibadala na Usanifu wa Mkabala
- Awamu ya Nne - Utekelezaji na Upimaji.
- Awamu ya Tano - Kagua, Rekebisha na Panua Wigo

Mkabala huu unakusudiwa kutumika kwa wadau wote wa EUWAWA wanaohusishwa katika kuboresha mifumo katika nchi zao. Ni hati hai, zana na uzoefu vinaweza kushirikishwa na watumiaji wote katika nchi zote. Zana hii inaunganisha na bidhaa zingine za *DVV International* kama vile *Curriculum globALE* na *Curriculum institutionALE.*

Yaliyomo katika kijitabu cha kwanza yanampa mtumiaji muhtasari wa mbinu. Maelezo ya dhana na michakato yametiwa ndani zaidi katika vijitabu vilivyosalia, kulingana na kila awamu ya mbinu. Hivyo, kijitabu cha kwanza kinatoa usuli kuhusu mantiki ya mbinu na jinsi ilivyotengenezwa. Kinaweka kanuni za msingi zinazounda msingi wa kuelewa mbinu. Msingi wa kinadharia na ulinganisho na mbinu zinazofanana husaidia kuiweka MKMEUWAWA ndani ya mazungumzo na mazoezi ya EUWAWA. Kijitabu hiki pia kinatoa muhtasari wa mfumo wa dhana na awamu za mkabala, majukumu na wajibu wa wadau mbalimbali, na upeo na muktadha ambamo mbinu hiyo zinaweza kutumika. Inahitimisha kwa kuonesha athari kwa mashirika yanayopenda kutumia mbinu na miongozo ya kutumia Seti ya Zana.

# 2. USULI NA MADHUMUNI

***"Namna zote za kujifunza na kutaka mabadiliko huanza na namna fulani ya kutoridhika au kuchanganyikiwa"***

Kurt Lewin kama ilivyonukuliwa na: (Schein, Vol 1, Number 1)

**Kwa mujibu wa Taarifa ya 4 ya Dunia Kuhusu Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima ya UNESCO, karibu katika theluthi ya nchi zote, chini ya asilimia tano ya watu wazima wa umri wa miaka 15 na zaidi, ndiyo wanaoshiriki katika programu za elimu na ujifunzaji. Baadhi ya nchi zinaweza kutoa taarifa ya maendeleo zaidi, ingawa bado inadhihirika kwamba sehemu nyingi duniani ujifunzaji wa watu wazima hauko mahali ambako panatarajiwa. Changamoto zifuatazo zinaendelea kujitokeza (UNESCO Institute for Lifelong Learning, 2019):**

- Ushiriki hafifu wa makundi yaliyotengwa na yaliyo katika mazingira magumu, hasa wale walionyimwa nafasi ya kupata fursa za ujifunzaji bila ukomo. Hili linaathiri moja kwa moja kazi za riziki na stadi za maisha wanazohitaji ili kuishi katika ulimwengu wenye uchangamano unaoongezeka.
- Mifumo hafifu ya ukusanyaji wa data, ufuatiliaji na tathmini inayomaanisha kwamba hatujui ni akina nani wanaoshiriki, ubora wa programu ukoje, hivyo, mabadiliko na maboresho gani yanahitajika.
- Ingawa nchi nyingi zimetunga na kuidhinisha sera mpya za EUWAWA, sera hizi hazijapanuliwa au hazijasambazwa nchi nzima pamoja na mifumo muhimu ya kiutawala ili kuwezesha utekelezaji wake.
- Fedha za kugharimia EUWAWA bado hazitoshi katika nchi zilizo nyingi.

Bara la Afrika, linakabiliwa na changamoto za mahitaji ya elimu na maisha kwa sababu ya ongezeko la watu. Hata baada ya kufanyika kwa juhudi kadhaa za kupambana na ujinga wa kutojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watu wazima kwa miongo kadhaa iliyopita, viwango vya ujinga vinaendelea kuwa juu, tena kukiwa na kutofautiana kijinsia na kati ya mijini na vijijini. Ongezeko la dhati la utoaji wa elimumsingi kwa wote linaweza kutatua tatizo hili kadiri muda unavyokwenda. Hata hivyo, viwango vilivyopo vya wanaoacha shule vinaendelea kutengeneza makundi ya vijana na watu wazima wasiojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, wanaojua kidogo Kusoma na Kuandika na wasio na ujuzi au wenye ujuzi kidogo ambao wana fursa finyu za kutengeneza maisha bora.

Mahitaji ya kuwekeza katika elimu na ujifunzaji wa watu wazima yanaendelea kuwapo. Wakati uhusiano kati ya elimu na kupungua kwa umasikini ukifahamika kwa muda mrefu, ushawishi wa kisiasa bado haujafanikiwa. Bado kuna hali ya kukosekana kwa uelewa wa wazi wa dhana kuhusu upana wa sekta ya EUWAWA na jinsi ya kuchangamanisha kisomo cha watu wazima na mafunzo ya stadi nje ya mfumo rasmi, stadi za ufundi na stadi za maisha n.k. Kila wahusika wanakazia utofauti katika misingi, malengo na vitendo badala ya kuweka muunganiko na kutafuta ushirikiano mtambuko. Sekta hii imeendelea kuwa na weledi wa viwango vya chini na yenye masharti hafifu ya ajira ambayo hatimaye yameathiri ubora wa elimu inayotolewa.

Shirika la Kimataifa la DVV Ukanda wa Mashariki/Pembe ya Afrika, hususani ofisi za nchi za Ethiopia na Uganda pamoja na serikali washirika, walianza kuuliza maswali kama vile:

- Kwa nini viwango vya kutojua Kusoma Kuandika na Kuhesabu na vya umasikini vinaendelea kuwa juu katika nchi nyingi za Afrika licha ya kuwapo kwa programu za kitaifa za elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi?
- Kwa nini jitihada za serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali hazijabadili takwimu hizo?
- Ni jinsi gani tunaweza kufasili elimu na ujifunzaji wa watu wazima katika namna yenye uchangamani?
- Kwa nini mfumo wa elimu na ujifunzaji wa watu wazima unaonekana kushindwa kutoa huduma bora kwa makundi ya walengwa wake?
- Mfumo wa elimu na ujifunzaji wa watu wazima unajumuisha vitu gani? Sehemu zake ni zipi na zinahusianaje?
- Tunapimaje maendeleo katika ujenzi wa mfumo wa elimu na ujifunzaji wa watu wazima?
- Ni ofisi zipi za sekta za serikali, wadau na wahusika wengine wanaoshirikishwa na majukumu yao na wajibu wao ni upi?
- Je, kazi ya sasa ya serikali, Shirika la Kimataifa la DVV na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali vinachangia kuleta mfumo endelevu unaoweza kutoa huduma zinazotakiwa?
- Je, maeneo ya kuanzia yanapaswa kuwa yapi katika kujenga na kuimarisha mfumo uliopo wa elimu ya watu wazima?
- Ni awamu zipi zinazohusika katika kujenga mfumo endelevu wa elimu ya watu wazima kadiri muda unavyokwenda?

Kupitia mfululizo wa warsha za majadiliano, michakato na mikutano, tulitambua kwamba, kama ilivyo kwa wadau wengine wengi, jitihada zetu za kutegemea sehemu ya ufundi ya elimu ya watu wazima hazitoshi na hazijikiti katika kushughulikia mzizi wa tatizo la udhaifu wa utoaji wa elimu na ujifunzaji wa watu wazima na utoaji wa huduma zake. Kuwapo kwa sera na mkakati hakutoshi kuleta uhakika wa utoaji wa huduma bora na zinazoendana na mahitaji kwa makundi ya walengwa. Kutoa mafunzo kwa wakufunzi na wawezeshaji, kuunda mtaala mpya.

na vifaa ni hatua muhimu katika kuimarisha ubora wa huduma hizo. Lakini, hayo hayatakuwa na matokeo mazuri mpaka kuwapo na muundo wa kiutawala ulioidhinishwa, wenye watumishi wa kutosha na unaogharimiwa ili uweze kuendeleza utoaji wa huduma hizi. Inaonekana kama jitihada zilizopo sasa mara nyingi zinashughulikia tu matokeo ya uwapo wa mfumo dhaifu uliopo katika elimu ya watu wazima, badala ya kushughulikia mzizi wa tatizo.

Tuligundua kwamba elimu na ujifunzaji wa watu wazima kwa mapana yake, kama mfumo wenye uchangamani, haipewi umakini wa kutosha. Taarifa kuhusu sera, utawala, ugharimiaji, uundaji wa mitaala, vifaa vya kufanyia mafunzo na uendeshaji wa mafunzo vinaweza kupatikana katika maandiko na taarifa za utekelezaji. **Kinachokosekana ni kiunzi kipana cha dhana ambacho kinaweka pamoja vipengele vyote hivyo katika namna ya kimfumo kwa kusudi kuu la kutoa huduma bora za elimu na ujifunzaji wa watu wazima.** Hili lilisababisha kufanya kazi ya kuchunguza mtazamo na mikabala ya kimfumo ili kuelewa zaidi mfumo unaoweza kutumika na namna unavyoweza kufanya kazi. Hali hiyo ya elimu na ujifunzaji wa watu wazima kuwa tata na mtambuko ilileta msukumo wa kutaka kuchunguza mikabala na mifano mbalimbali ya kidhana.

Huu mfumo wa ruwaza wa dhana unaitaka timu ya kikanda ya Shirika la Kimataifa la DVV na washirika kupiga hatua na kutoka nje ya wigo wa elimu ya watu wazima na kuchukua dhana na mawazo kutoka kwenye fikira za kimfumo, uongozi wa umma, maendeleo ya shirika na mambo ya utawala. Kadiri muda ulivyopita, mkabala mpya wa kazi hii uliibuka kimfumo, ukiwa na mafunzo ya kujifunza katika kila hatua. Hili lilihitimisha katika kukuza Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (MKMEUWAWA), ukiwa na malengo yafuatayo:

- Kuzifanya huduma za elimu na ujifunzaji wa watu wazima kuwa bora. Utoaji wa huduma ndilo kusudi kuu la mfumo unaofanya kazi. Msisitizo unakuwa kwenye jamii inayohitaji huduma hiyo.
- Kupata kiunzi cha dhana cha jumla kinachoweza kuwasaidia wadau kuelewa na kujenga mfumo wa EUWAWA kwa utaratibu endelevu katika awamu zote mbalimbali.



# 3. MCHAKATO NA MBINU ZA KUENDELEZA MKABALA HUU

***“Huwezi kuuelewa mfumo hadi utakapojaribu kuubadili”***

Kurt Lewin kama alivyonukuliwa na Schein: (Schein, Vol. 1, No. 1)

**Mchakato wa kukuza MKMEUWAWA ulianza mwaka 2014 na ulihusisha mfululizo wa matukio, warsha, mikutano na fursa za tafakuri, pamoja na kazi za kuendelea zilizokuwa sehemu ya utekelezaji wa mradi wa Shirika la Kimataifa la DVV nchini Ethiopia na Uganda. Uzoefu kutoka katika nchi hizo mbili ulisaidia kuzijaribu, kuongezea na kuendeleza dhana na zana mbalimbali. Kadiri Ukanda wa Mashariki/ Pembe ya Afrika ulivyoanza kuyashirikisha uzoevu maeneo mengine jirani ya Afrika, mapenzi kwa mkabala huo yalikuwa na kusababisha warsha ya mafunzo ya Afrika kuhusu Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima mwaka 2019. Warsha hiyo ilizihamasisha nchi kadhaa za Afrika kuufuata mkabala huo na ilitoa fursa ya kuimarisha zaidi MKMEUWAWA ikija pamoja na uzoefu anuwai na zana za kutumia.**

Mbinu iliyotumika kuendeleza mkabala huo imejikita kwenye vitendo shirikishi vya ujifunzaji na utafiti. Mambo yaliyofundishwa kutokana na matukio haya na utekelezaji wa programu/miradi, yakiunganishwa na utafiti wa mazungumzo katika maeneo tofauti kama vile: Uongozi wa Umma, Maendeleo ya Kiasasi na Elimu ya Watu Wazima, yanaendelea kuhimiza maendeleo zaidi ya mkabala huo.

Dhana ya utafiti/ujifunzaji kwa vitendo inamaanisha juhudi za mtendaji kuelewa vizuri yale yanayoendelea katika mazingira ya kujifunzia na ya kazi. Ingawa kwa miaka kadhaa aina mbalimbali zimepatikana, mikabala mingi imechukua mwelekeo wa kimbinu na kijumuishi ambao unatumia utambuzi wa tatizo, kupanga utendaji, utekelezaji, tathmini na tafakuri. Uzoefu wa kujifunza, pamoja na maarifa yaliyopatikana katika mzunguko wa kwanza yanatoa mwelekeo wa mzunguko wa pili, huku mpango kazi na utekelezaji vikiwa vimerekebishwa kadiri mchakato unavyojirudia. Mchakato pia una sifa ya uwezeshaji wa washiriki, ushirikiano kupitia ushiriki, kupata ujuzi na maarifa na hatimaye mabadiliko katika vitendo na mazingira, n.k. Watendaji siyo tu kwamba hutafuta njia za kuboresha utendaji wao katikati ya vikwazo mbalimbali katika mazingira wanamofanya kazi, pia huwa mawakala muhimu wa mabadiliko na kutangaza ujifunzaji wao kwa umma (Cilliers, n.d.).

Sifa na kanuni hizi zimezingatiwa katika mchakato wa kutengeneza MKMEUWAWA. Lengo la mwanzo lilikuwa ni kuboresha mifumo ya EUWAWA katika Ukanda wa Mashariki/Pembe ya Afrika. Lakini baada ya muda, kadiri ujifunzaji na utendaji ulivyoendelea faida nyingine zilionekana wazi na mkabala kamili wa mifumo ya kujenga ujifunzaji na elimu ya watu wazima uliibuka. Mkabala na seti ya zana vinanufaika kutokana na nadharia na vitendo. Mkabala haulengi kuwa nyenzo ya kitaaluma, ila mkabala wa vitendo wenye mbinu na zana zinazoweza kuboresha utoaji wa huduma ya EUWAWA.

# 4. KANUNI ZA MSINGI NA MAZINGATIO

**Katika kiini cha MKMEUWW kuna mfululizo wa kanuni za msingi na mazingatio ambayo yanaathiri namna mkabala unavyofahamika na kutumiwa. Kanuni hizi zimeungana na kwa ufupi zimebainishwa na kufafanuliwa hapa chini:**

## Mkabala unaojali haki ya maendeleo, elimu na ujifunzaji kwa watu wazima

MKMEUWAWA unaielezea EUWAWA kama haki na utatumia mkabala unaojali haki katika utoaji wa huduma ya EUWAWA. Matumizi ya mkabala unaojali haki yanahamisha namna tunavyoifikiria EUWAWA na maendeleo na namna tunavyoshughulikia changamoto ndani ya mfumo wa utoaji huduma. Katika kukiita kitu fulani kwenye haki ya binadamu, kuna maana ya harakaharaka inayokuja na kudokeza kwamba watu wote wana haki sawa ya kupata huduma hiyo. Hivyo mtu yeyote anao wajibu wa kutimiza haki hiyo na anaweza kuwajibishwa ili kuitoa (Lindsey, 2006). Kwa hiyo, MKMEUWAWA pia unarejelea huduma ya EUWAWA sawasawa na utoaji wa EUWAWA. Huduma zina mtazamo zaidi kwamba ni wajibu wa dola na asasi za kiraia.

Mkabala unaojali haki hutofautisha kati ya wanaostahili haki (mtu mmojammoja, makundi yenye madai halali ya EUWAWA kama haki) na watimiza haki wanaojumuisha dola/serikali na watendaji wasio wa serikali. Lengo ni kwamba badala ya haki kutolewa pale tu inapokuwa inapatikana, elimu ni haki iliyohakikishwa ambayo ni lazima itolewe na watimiza haki (Avramovska, 2015).

MKMEUWAWA unatambua watendaji wote wa serikali na wasio wa serikali kama watimiza haki; lakini unaitambua serikali kama mtimiza haki mkuu kwa mujibu wa sheria za kitaifa na kimataifa. Mantiki yake ni kwamba watendaji wasio wa serikali, hasa watendaji wa asasi za kiraia, wakati wote hawana rasilimali za kutoa huduma hizo kiuendelevu, kipekee kwa idadi kubwa ya vijana na watu wazima nchini. Majukumu na wajibu wa watimiza haki hawa yanatofautiana kati ya nchi na nchi na yanapaswa kupatikana katika Awamu ya Kwanza ya mkabala (Kujenga Makubaliano) ili kutambua ni jukumu gani kila mtendaji atalitimiza katika kujenga mfumo wa EUWAWA.

## Uchangamani

Muundo wa miradi/programu na huduma za EUWAWA zinazotolewa kwa hatua hizi mara nyingi hufanyika kwa namna ya uchangamani. Kwa mfano, zinaweza kujumuisha kisomo chenye manufaa kwa watu wazima na maendeleo ya jamii, na mafunzo ya stadi za kujikimu, n.k. Asili changamani ya huduma hizi mara nyingi huhitaji ushiriki wa utaalamu wa zaidi ya sekta moja – na hivyo huhitaji watendaji kutoka sekta mbalimbali za serikali na/au asasi zisizo za serikali (AZISE). Asili mtambuko ya ujifunzaji na elimu ya watu wazima imetambuliwa katika muundo na utekelezaji wa MKMEUWAWA na imerejelewa kama 'uchangamani mlalo' katika sekta mbalimbali.

Utoaji wa huduma za EUWAWA unaweza kuibuka kutoka kwenye sera na/au mkakati wa kitaifa, lakini hatimaye inatolewa katika ngazi ya serikali za mitaa na katika jamii. Hii inamaanisha kwamba utoaji wa huduma unatakiwa kueleweka katika maeneo au ngazi zote za mfumo wa utawala wa nchi. Hili linarejelewa kama 'uchangamani wima' katika muktadha wa MKMEUWAWA.

## Ngazi ya chini-kati-juu

Istilahi hii imenasibishwa na mkabala wa Shirika la Kimataifa la DVV wa kubuni muundo lakini pia unatumiwa na watendaji wengine. Ngazi ya juu inaeleweka kuwa ngazi ambapo sera na mikakati inabuniwa na kutungwa ikiambatana na miongozo yake, upangaji bajeti, n.k. Hii kwa kawaida, hufanyika katika ngazi ya taifa, kulingana na muundo wa utawala wa nchi. Ngazi ya kati inarejelea aina zote za kuwajengea uwezo watendaji (katika muktadha wa Shirika la Kimataifa la DVV) na mara nyingi ni ngazi ambapo sera na mikakati hutafsiriwa na kuingizwa katika muundo wa programu/miradi ili kutoa huduma. Kwa kawaida, hii hufanyika katika ngazi ya chini katika mfumo wa utawala, mfano ngazi ya jimbo, mkoa au wilaya. Ngazi ya chini inaeleweka kuwa ni ngazi ambapo huduma zinatolewa na ndiyo kuna mwingiliano kati ya utoaji (utoaji huduma) na upande wa kuhitaji huduma (watumia huduma). Hii kwa kawaida hujumuisha ngazi za chini za watendaji wa serikali za mitaa.

## Ushawishi wenye Ushahidi

Miradi ya majaribio mara nyingi inaweza kutoa ushahidi kwamba mbinu au mkabala mpya unafaa sana, una matokeo na uwezekano wa kupanuliwa kwa kundi kubwa la EUWAWA au maeneo ya kijiografia. Pia, ina uwezekanao wa kushawishi utungaji wa sera na mikakati. Kutokana na uzoefu kutoka Ukanda wa Mashariki/Pembe ya Afrika, MKMEUWAWA unafuata kanuni hii ilimradi mahitaji yafuatayo yatimizwe:

- Kwamba ili ushawishi wenye ushahidi uwe na mafanikio, wadau na wahusika wote wahusishwe na kushirikishwa tangu mwanzo wa mradi. Siyo tu kama watazamaji mwishoni mwa mradi bali kama washiriki wenye majukumu na wajibu wakati wa utekelezaji wa mradi.

- Fursa lazima itengenezwe kwa ajili ya tafakuri na marekebisho ya papo kwa papo katika awamu ya majaribio/utekelezaji.
- Njia za mawasiliano na mrejesho lazima zitengenezwe katika sekta zote na ngazi zote za utawala/utekelezaji.
- Ujifunzaji kwa vitendo kwa tafakuri muhimu unapaswa kuwa sehemu muhimu ya mchakato.

### Ushiriki, ubia na umiliki

Ushiriki, ubia na umiliki ni kanuni muhimu zilizopachikwa ndani ya MKMEUWAWA. Wadau wote wanaohusika katika kujenga mfumo ni washiriki na wabia katika mchakato. Hakuna watazamaji wala wateja. Katika mwelekeo kwa kujifunza kwa vitendo shirikishi, mkabala wa kujenga mfumo huchukua sura ya kuchunguza kwa pamoja, kujitafakari kunakofanywa na wadau wote walioshiriki katika awamu zote za mkabala. Wadau wanafanya upimaji kwa njia ya upitiaji taalimu na kujifunza kutokana na kupitia uchunguzi muhimu wa ushirikiano. Wanamiliki matokeo ya upimaji wa mfumo na kwa pamoja huchambua machaguo mbadala ya kusanifu na kuboresha mfumo. Bila ushiriki na umiliki huu, kunyosheana vidole na lawama hutokea na kupunguza fursa ya kujenga mfumo wa mkabala mpya na shirikishi wa EUWAWA. Matumizi ya wataalamu washauri yanapunguzwa na hata hivyo wanapewa majukumu ya uwezeshaji na usaidizi. Vinginevyo wadau wataendesha mchakato wa kujenga mfumo na kuipima mifumo yenyewe, mara nyingi matokeo hayaaminiki na watapata shida kushiriki katika utatuzi wa matatizo kibunifu. Wadau hawana budi kuwa waleta mabadiliko katika mchakato.

### Kujenga uwezo

Wadau wote wanapaswa kupewa mafunzo na kuelekezwa kuhusu MKMEUWAWA na kanuni zake za msingi, kuelewa dhana, zana na michakato ili kutimiza wajibu wao katika shughuli za kila awamu. Kazi ya kuwajengea uwezo inasaidia kukuza umiliki, ushiriki na uendelevu. Kila awamu ya mkabala inahitaji stadi tofauti, hivyo lazima mafunzo yatolewe ipasavyo. Vitabu vilivyobaki katika Seti ya Zana vinatoa maudhui na miongozo ya mafunzo haya.

### Uendelevu

Lengo la kujenga mfumo wa EUWAWA ni kutengeneza mfumo endelevu unaoweza kutoa huduma. Uendelevu unaweza kupimwa katika ngazi tofauti kwa kutathmini masuala yafuatayo:

- Ni kwa kiwango gani sera, mikakati na sheria zinahakikisha haki ya EUWAWA inapatikana?
- Ni kwa kiwango gani huduma za EUWAWA zinapangwa na kutengewa bajeti kwa mipango ya maendeleo ya kitaifa na sekta?
- Je, taasisi zinazoshughulikia huduma za EUWAWA zina uwezo wa rasilimali watu na wa kitaasisi kutoa huduma kwa makundi yote lengwa kwa muda?
- Je, huduma hizo zinafaa, zinapatika na zinatolewa kwa ubora unaotakiwa ili kuwa na matokeo na kubadilisha maisha ya wanafunzi watu wazima?

# 5. VIASHIRIO KUHUSU NADHARIA NA ULINGANISHI

*“Hakuna kitu kinachotekelezeka kama nadharia nzuri”*

Lewin alivyonukuliwa na Schein, Vol. 1, No. 1).

**Uwezo mkubwa umo katika kuuleta Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (MKMEUWAWA) karibu kabisa na mjadala unaofanyika katika maeneo mengine ya kisera na kinadharia, hasa pale mjadala unapogusa ujifunzaji na elimu ya watu wazima (EUWAWA) kama sekta ndogo ya mfumo wa elimu na kipengele muhimu cha Ujifunzaji bila Kikomo.**

Katika zama hizi za utandawazi na kidijiti ipo haja ya kuhakikisha kwamba elimu kama haki ya binadamu inaangaliwa kwa mtazamo wa ujifunzaji bila kikomo kwa wote. Hii inajumuisha EUWAWA kwa vijana, watu wazima na wazee. Siku zijazo wakati ujifunzaji bila kikomo itakapotambuliwa kama haki ya binadamu EUWAWA itaibuka kama kipengele muhimu cha haki hii (Dunbar, 2020). Ahadi za kitaifa na kimataifa zilizotolewa hadi sasa na kwa kiwango ambacho EUWAWA imetambuliwa kama utaalamu na taaluma ni ushahidi wa maendeleo yaliyopatikana japo changamoto zinaendelea kuwapo. Utaasisishaji wa EUWAWA unabaki kuwa wa muhimu sana ili kuhakikisha kwamba EUWAWA inadaiwa kama haki.

## Mhamo wa ruwaza kwenda ujifunzaji bila kikomo

Kwa mujibu wa UNESCO: “Ujifunzaji wa maisha yote umekita mizizi yake katika uchangamani wa kujifunza na kuishi. Unajumuisha shughuli za ujifunzaji kwa watu wa kila umri (watoto, vijana, watu wazima na wazee) katika mazingira yote ya maisha (familia, shule, jumuiya na mahali pa kazi, n.k.), na kupitia njia mbalimbali (rasmi, nje ya mfumo rasmi na isiyo rasmi) ambazo kwa pamoja hutosheleza haja na mahitaji mbalimbali ya kujifunza. Mfumo wa elimu unaokuza ujifunzaji wa maisha yote unatumia mkabala jumuishi na unaogusa sekta zote na kuhusisha sekta zote ndogo na ngazi za elimu ili kuhakikisha utoaji wa fursa za kujifunza kwa watu wote mmojammoja” (UIL, 2010).

Maana hii inaendana na mhamo muhimu wa ruwaza kutoka elimu kwenda ujifunzaji ambao umetokea katika nyanja ya sera za kimataifa katika miongo ya hivi karibuni. Mwaka 1990, Tamko la Dunia la Elimu kwa Wote lilipitishwa huko Jomtien (UNESCO, 1990). Muongo mmoja baadaye mwaka 2000 Mkutano wa Elimu Duniani ulihitimishwa kwa Mwongozo wa Utekelezaji wa Elimu kwa Wote wa Dakar kwa kipindi cha 2000 – 2015 (UNESCO, 2000). Katika kipindi kilichotangulia, Asasi ya Ushirikiano wa Uchumi na Maendeleo (OECD) ilichapisha Ujifunzaji bila Kikomo kwa Wote (OECD, 1996), na UNESCO ilitoa ripoti ya Tume ya Delors kuhusu Ujifunzaji: Hazina ya Ndani (Delors, 1996). Wakati Benki ya Dunia ilipochapisha Mkakati wake mpya wa Elimu wa 2020 waliuita Ujifunzaji wa Wote. Kuwekeza katika Maarifa na Stadi za Watu ili Kukuza Maendeleo (World Bank, 2011).

Mhamo wa ruwaza kwenda ujifunzaji unaweka msisitizo mpya katika kuimarisha EUWAWA kama mfumo na sekta ndogo ya elimu. EUWAWA inaweza kufanikiwa kwa kiwango kikubwa tu iwapo ina taratibu za utawala na mifumo saidizi inayofanana na ya sekta zingine ndogo katika mfumo wa elimu, kama vile shule, ufundi stadi au elimu ya juu. Hata hivyo, EUWAWA inahitaji kanuni, sera, sheria na bajeti yake ili kufanya kazi vizuri kivitendo, kutengeneza na kuendeleza fursa za elimu na ujifunzaji wa watu wazima katika nyanja zote za maisha na kazi.

## EUWAWA kama kipengele muhimu cha ujifunzaji bila kikomo

EUWAWA ina sifa ya utofauti katika upeo, maudhui, programu, washiriki, utawala na miundo. Utofauti huo pia unaonekana katika ngazi za chini za kuipa EUWAWA mfumo wa kitaasisi na kitaalamu kutegemeana na maendeleo ya kihistoria na kiutamaduni katika nchi na mikoa/kanda zinazohusika.

Hata misamiati unaotumika duniani kote unatofautiana, na hubadilika baada ya muda, zikiwamo njia za ujifunzaji rasmi, nje ya mfumo rasmi na usio rasmi (Rogers, 2014). Utofauti huu ni mpana zaidi kuliko ule wa shule na vyuo vikuu, na unakaribiana zaidi ya utofauti wa aina za Elimu na Mafunzo ya Ufundi (EMAU). Hata hivyo, maeneo na nyanja zote hizi za elimu, ujifunzaji na mafunzo ni sehemu ya usomaji bila kikomo na lazima zionekane kuwa  ni sekta ndogo za elimu zenye umuhimu sawa. UNESCO inafafanua EUWAWA kama: “Kipengele muhimu cha ujifunzaji wa maisha yote. Inajumuisha aina zote za elimu na ujifunzaji zinazolenga kuhakikisha kwamba watu wazima wote wanashiriki katika jamii zao na ulimwengu wa kazi.

Inaashiria mfumo mzima wa michakato ya ujifunzaji, rasmi, nje ya mfumo rasmi na usio rasmi, ambapo EUWAWA wanaochukuliwa kama watu wazima na jamii wanamoishi, hupata na kuimarisha uwezo wao wa kuishi na kufanya kazi, kwa maslahi yao wenyewe na yale ya jumuiya, asasi na jamii zao. Ujifunzaji na elimu ya watu wazima hujumuisha shughuli na michakato endelevu ya kupata, kutambua, kubadilishana na kupitisha uwezo. Ikizingatiwa kwamba mipaka ya ujana na utu uzima inabadilika katika tamaduni nyingi, katika muktadha huu neno ‘mtu mzima’ linaashiria wale wote wanaohusika katika ujifunzaji na elimu ya watu wazima, hata kama hawajafikia umri wa kisheria wa ukomavu” (UNESCO, 2015b).

Mabadiliko ya idadi ya watu yanaonyesha kuwa watu wengi sasa wanaishi muda mrefu zaidi. Mabadiliko ya kiteknolojia yanataka maarifa, umahiri, na stadi tulizonazo ziendelee kuboreshwa. Mabadiliko ya kijamii na kiutamaduni yanatudai kuangalia kwa umakini mkubwa mitazamo, mienendo na tunu kwa mtazamo wa ujifunzaji wa maisha yote. Hivyo, EUWAWA itahitaji kupata kiwango cha juu cha umakini, utolewaji, na usaidizi ndani na nje ya mfumo wa elimu. Hamasa, utayari na sifa za kujifunza katika maisha yote vimewekwa vizuri mapema iwezekanavyo. EUWAWA inaweza kufidia kile ambacho hakikufundishwa mapema katika maisha. Fursa nyingine zote za ziada za ujifunzaji katika maisha ya utu uzima ni muhimu pia kuzizingatia. Inafaa kutazama ujenzi wa viunzi, kushinda vikwazo, kuwezesha muunganiko na kuhusiana, siyo tu ndani ya mfumo wa elimu, lakini pia kwenye maeneo na sekta nyingine muhimu za maisha na kazi kwa mtu na jamii.

### Ahadi za kitaifa na kimataifa

Kila nchi itatakiwa kutafuta namna yake ya kuanzisha mfumo wake wa sekta ndogo ya EUWAWA ndani ya mfumo wake wa elimu na mwelekeo wa ujifunzaji bila kikomo. Hata hivyo, nchi zote ni sehemu ya Umoja wa Mataifa (UN) na wanachama wa UNESCO ambapo zote zinatia ushawishi katika utungaji wa sera za elimu. Mwaka 1949, UNESCO ilianzisha mfululizo wa Mikutano ya Dunia kuhusu Elimu ya Watu Wazima (CONFINTEA).

Mwaka 1972 mfululizo wa mikutano hii uliofanyika Tokyo (CONFINTEA III) ulisaidia kufafanua vipengele vya EUWAWA kama taaluma. Zaidi ya mahitaji ya miundo ya kiutawala kupitia sera, sheria na fedha, mapendekezo ya kiuongozi na kimpangilio, mipango na mitaala, nyenzo na media vilitengenezwa, na mijadala ya mwanzo ilifanywa kuhusu kuwa sekta ya kitaasisi na kitaalamu. Mwaka 2009, CONFENTIA ya IV ulishuhudia nchi wanachama zikipitisha Mkakati wa Utendaji wa Belem, ambao ulifafanua maeneo matano muhimu, yakiwamo sera, utawala, fedha, ushiriki na ubora, ili kuwapo na ufuatiliaji wa mara kwa mara utakaofanywa na Taasisi ya UNESCO ya Ujifunzaji wa Maisha Yote kupitia Ripoti ya Dunia kuhusu Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (UIL, 2010).

Kwa kuangalia mafanikio ya wakati uliopita na changamoto za wakati ujao, mkutano wa Jukwaa la Elimu Duniani, uliofanyika mwaka 2015 huko Incheon, ulikuja na Ajenda ya Elimu 2030, ambayo pia ilikuwa imechangamana kabisa kama lengo la 4 katika Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu (MME). Malengo hayo 17 yalipitishwa na Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo Endelevu ili “kuhakikisha fursa sawa na bora za elimu na kukuza ujifunzaji wa maisha yote kwa wote” (UNESCO, 2015a). Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu (MME) yalikubaliwa na nchi zote wanachama wa Umoja wa Mataifa, na utekelezaji wake ni sehemu ya mipango ya kitaifa ya elimu pamoja na ushirikiano wa kimataifa.

EUWAWA iliratibiwa zaidi mwaka 2015 katika mapendekezo kuhusu Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (EUWAWA) yaliyopitishwa katika Mkutano Mkuu wa UNESCO na nchi zote wanachama wa UNESCO (UNESCO, 2015b). Serikali zinapaswa kufanya kila linalowezekana kuhakikisha utimilifu na kuwezesha utekelezaji. Asasi zisizo za serikali zinaweza kusaidia, wakati huohuo kuziwajibisha serikali zao na asasi za kimataifa. Mapendekezo kuhusu Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima yanajumuisha dhana ya wazi ya jumla kuhusu michakato ya kuifanya EUWAWA ya kitaasisi na kitaalamu. Hata hivyo, mapendekezo yanahitaji marekebisho ili kufaa katika miktadha tofautitofauti:

- Kuweka au kuimarisha miundo ya kitaasisi kama vituo vya ujifunzaji katika jamii, kwa ajili ya kutoa EUWAWA na kuwahamasisha watu wazima kuvitumia kama vitovu vya mtu mmojammoja kujifunza na kwa ajili ya kuleta maendeleo ya jamii.
- Kuandaa maudhui mwafaka na njia za kujifunzia, labda hasa kwa kutumia lugha mama, kama lugha ya kujifunzia na kufundishia na kutumia uwezeshaji ambao mwanafunzi ndiye kitovu chake, ikisaidiwa na teknolojia ya habari na mawasiliano, na rasilimali huria za elimu.
- Kuboresha mafunzo, kujenga uwezo, masharti ya ajira na kuwapatia utaalamu wawezeshaji wa watu wazima (UNESCO, 2015c, kur. 4-5).

### Ujifunzaji bila Kikomo, EUWAWA na Sekta isiyo Rasmi

Vijana na watu wazima katika sekta isiyo rasmi wanakosa fursa za elimu rasmi au ujifunzaji bila kikomo nje ya mfumo rasmi. EUWAWA bado ni kama ndugu maskini kama sekta ndogo ya mfumo wa elimu. Katika nchi nyingi EUWAWA haiongozwi na sera, sheria na bajeti yoyote thabiti, hasa kwa wale walioachwa pembezoni na wanaofanya kazi katika mfumo usio rasmi. “Utawala na sera zinazohusu ujifunzaji wa maisha yote katika uchumi usio rasmi,

vinakabiliana na changamoto mbili na zinazoingiliana kutokana na asili mparaganyiko ya mfumo unaoshughulika na masuala yanayogusa maisha yote na kona zote za maisha. Hili linachagizwa na changamoto ya nyongeza ya kujaribu kushughulikia muktadha usio rasmi kupitia zana za kiutawala na kisera pamoja na mikabala ambayo kimsingi ni rasmi. Ukubwa hasa wa uchumi usio rasmi – watu bilioni 2 – na asili yake mchanganyiko inamaanisha wapo katika miktadha mbalimbali katika nchi na kanda mbalimbali" (Palmer, 2020, uk.50).

Katika kujaribu kuiwasilisha MKMEUWAWA kwa jamii kubwa ya wataalamu katika serikali, asasi zisizo za serikali na wasomi, inasaidia kutumia matokeo ya utafiti kwa kutazama aina mpya za uongozi wa elimu au usimamizi wa umma. Hapa, serikali inabaki kuwa muhimu katika ngazi zote, ila siyo peke yake, na sio tu kwa njia ya maagizo kutoka juu kwenda ngazi za chini. Zaidi ya njia za mpangilio wa madaraka, utendaji mlalo wa mitandao au mikoa ya ujifunzaji katika jamii za wenyeji ndani ya vijiji au miji ya ujifunzaji inazidi kuongezeka. Mitazamo mingine lazima iheshimiwe, mfano kuhusu uongozi wa elimu ambapo mgawanyo wa serikali na soko unapotea kwa sababu ya ubia mbalimbali kati ya serikali na sekta binafsi ambazo zinajumuisha majukumu muhimu ya asasi za kiraia na mipango ya jamii husika.

### EUWAWA kama utaalamu na uga wa taaluma

Nchi nyingi zimefanya mpango katika mazingira na mifumo ya kitaasisi ambayo inaweza kusaidia mipango ya kijamii ya EUWAWA. Kuna vituo vingi vya kujifunzia katika jamii vyenye majina na kazi tofauti vinavyogharimiwa na serikali za mitaa au na mashirika ya hiari. Makampuni makubwa yana wafanyakazi wataalamu kwa ajili ya kuwafundisha wafanyakazi wao. Kuboresha umahiri na stadi mara nyingi pia hufanywa na wataalamu wa nje kutoka taasisi za mafunzo. Waajiriwa wenye sifa na wa kudumu hufanya kazi pamoja na wale wa muda mfupi, na watoa mafunzo zaidi huchanganya njia za analojia na dijitali kupitia ujifunzaji mchanganyiko. Katika nchi ambapo EUWAWA ni sehemu ya ujifunzaji bila kikomo na hupata msaada wa serikali, ushiriki zaidi na imara huhitaji utaalamu zaidi kama eneo muhimu la kuingilia kati kwa ajili ya maendeleo ya wasimamizi na wawezeshaji tarajali wa EUWAWA. Baadhi ya watahiniwa wanatakiwa kufundishwa kutambua, kuhalalisha na kuthibitisha EUWAWA waliojifunza kabla, wengine wanahitaji kufundishwa ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha ubora na kujulisha sera na matokeo. Kundi muhimu linajumuisha wale wanaotaka kuboresha maarifa yao ndani ya EUWAWA.

Elimu ya juu inaweza kusaidia kuandaa wawezeshaji wa baadaye wa elimu ya watu wazima. Vyuo vikuu vina masomo ya shahada ya kwanza na ya pili katika elimu zenye lengo, taratibu na ubobevu mbalimbali, baadhi hutoa fursa za shahada za uzamivu, pamoja na tafiti na mafunzo linganishi kuhusu EUWAWA. Inapendeza kwamba utaalamu huo ukitumiwa katika EUWAWA katika fani zake nyingi za utendaji, kama vile maendeleo ya jamii, kufundisha kisomo, kuendeleza asasi au rasilimali watu, mitazamo ya kimataifa au linganishi (international or comparative dimension), zimekuwa kipengele cha kawaida kama kuwafundisha walimu au wasimamizi wa shule. Shahada hizi za chuo kikuu kwa wawezeshaji wa elimu ya watu wazima zitakuwa muhimu kama masharti ya ajira hapo baadaye. Kazi ya utafiti kwa vyuo vikuu inapaswa kuwapo kwa ajili ya EUWAWA na ujifunzaji bila kikomo kwa mitazamo ya taaluma mbalimbali na mchango ili kuimarisha uwezo wake kama fani ya kitaaluma. Kwa muda huu, tafiti nyingi katika elimu zinahusiana na shule au elimu ya juu. Hali bado iko hivi katika nchi ambamo katika EUWAWA kuna watu wazima wengi kuliko vijana katika shule na vyuo vikuu. Hali iko hivyo kuhusiana na upatikanaji wa data na takwimu, ambapo za shule na elimu ya juu ziko tayari, lakini zile za EUWAWA ni mara chache hukusanywa na kutumiwa.

### EUWAWA kuwa ya kitaalamu na kitaasisi

MKMEUWAWA unao uwezo wa kuichambua na kuiweka EUWAWA ndani ya mfumo wa elimu kama sekta ndogo yenye utawala imara, yenye vyombo na taratibu za kuifanya kuwa ya kitaasisi na kitaalamu. Pia, kuna miongozo na vifaa vya kuikuza EUWAWA kama sekta ndogo. Mtaala wa Kimataifa (MK) umeandaliwa na Shirika la Kimataifa la DVV na washirika wake ili kuwafunza watendaji katika usimamizi, utawala na ufundishaji (Avramovska, 2015). MK umetafsiriwa katika lugha zaidi ya kumi na hivyo kuwapo kwa ajili ya matumizi katika mazingira mbalimbali. Hivi karibuni, Mtaala wa Taasisi (MT) umeongezwa kama zana ya kuchambua na kuendeleza zaidi mahitaji ya kitaasisi (Denys, 2020). Mitaala yote miwili ni muhimu katika ngazi za kati na chini, kwa njia hii pia husaidia ngazi ya juu.

Hatimaye, taasisi muhimu kwa wanafunzi watu wazima na washiriki ni zile zilizomo katika jumuiya zao. Pia, kuna mapendekezo kutoka ngazi ya kimataifa yaliyojumuishwa kwenye MME: "Kutengeneza mahali na mazingira ya kujifunzia elimu nje ya mfumo rasmi na elimu ya watu wazima na elimu ili ipatikane kwa mapana, ikiwamo mitandao ya vituo na mahali pa kujifunzia katika jamii, utoaji wa rasilimali za TEHAMA kama vipengele muhimu vya ujifunzaji wa maisha yote" (UNESCO, 2015a, uk. 52). Hili linaelekeza kwenye kuwapo kuchuja aina za ujifunzaji mchanganyiko ambapo taasisi na njia za ujifunzaji kidijitali zinatengenezwa kwa maslahi ya wanafunzi.

Wakati huohuo, ufafanuzi zaidi unatakiwa ili kufahamu tofauti kati ya taasisi mbalimbali za ngazi ya jamii, kama vile Vituo vya Elimu ya Watu Wazima (VEWW), Vituo vya Jamii vya Kujifunzia (VJK), Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (VMW), na sasa katika muktadha wa MT, pendekezo la kutumia Taasisi za Elimu ya Watu Wazima na Elimu (TEWWE). Mikabala kuhusiana na uanzishaji wa VJK nchini Ethiopia na Uganda imeripotiwa (DVV International East Africa Regional Office, 2020). Wakati wa mkutano wa kimataifa kuhusu VEWW na VJK, washiriki walikubaliana kuhusu ujumbe muhimu ambao zinaweza kutumiwa katika miktadha mbalimbali (DVV International, 2017 na Avramovska, 2015). Katika ngazi ya kati ya kujenga na kuimarisha mitandao, vyama, na mabaraza ya ushauri ya EUWAWA, inasaidia sana. Na katika nchi zingine, kuna taasisi za kitaifa zinazoshughulikia utafiti na maendeleo ya EUWAWA.

Tunachoweza kujifunza kutokana na mifano na uzoefu kutoka ulimwenguni kote ni kwamba EUWAWA inakuwa suala la kikatiba, kupitia sera mbalimbali, sheria na bajeti na kudai utoaji zaidi ni jambo lenye umuhimu mkubwa ili kuongeza ubora, ushiriki, na kutengeneza fursa sawa kwa vijana na watu wazima. Kwa mfano, nchini Ujerumani, sera, sheria na bajeti ya elimu, ikijumuisha EUWAWA, ipo chini ya mamlaka ya Länder (majimbo au mikoa). Volks-hochschulen (vhs), au shule za sekondari za juu, kwa Ujerumani zinaweza kuonekana sawa na Vituo vya Jamii vya Kujifunzia (VJK). Vituo hivi ni sehemu ya muundo wa utawala katika kijiji au mabaraza. Kwa kweli, vhs ni sehemu ya fursa za ujifunzaji bila kikomo kwa watu wazima (DVV International, 2011; (Hinzen, 2020).

# 6. DHANA ZA MKMEUWAWA, MUKTADHA NA MAJUKUMU YA WADAU

**Sehemu hii ya mwongozo inaandaa msingi wa kutambulisha kiunzi cha dhana cha MKMEUWAWA na awamu za mchakato. Imejikita zaidi katika vigezo vifuatavyo:**

- **Dhana muhimu zinazotumiwa na zinazozungumziwa ndani ya mkabala.**
- **Upeo na muktadha ambamo mkabala huu unaweza kutumiwa (mf. kisomo kwa watu wazima, na mafunzo ya ujuzi nje ya mfumo rasmi, n.k.)**
- **Wadau na watimiza majukumu watakaohusika katika mchakato.**

## 6.1 Kuelewa dhana

Zifuatazo ni dhana ambazo mara nyingi hurejelewa na kutumiwa katika Seti ya Zana za MKMEUWAWA.

### Vijana na watu wazima

Maana na umri wa vijana na watu wazima inatofautiana kati ya nchi na nchi na hakuna maana moja iliyokubaliwa. Kwa lengo la kitakwimu, Umoja wa Mataifa unaelezea vijana kuwa ni wale walio katika umri wa miaka 15 mpaka 24. Baadhi ya nchi zinaelezea kuwa vijana ni wale wenye umri wa miaka 18 mpaka 30. MKMEUWAWA unalenga kutoa huduma ya EUWAWA kwa watu wazima na vijana wenye umri wa miaka 15 na kuendelea. Mkabala huu unatambua makundi mbalimbali ya wanafunzi ambao wanaweza kuwa na masilahi, mahitaji, pia upangaji na utekelezaji wa huduma unaweza kutakiwa kurekebiswa ipasavyo.

### Kujenga mfumo

Zipo fasili nyingi za mfumo, kwa mfano:

- Mfumo ni seti ya michakato mbalimbali ambamo uhusiano wa sababu na athari unaweza kupatikana.
- Mfumo hujumuisha safu za dhana au vipengele vinavyotakiwa ili kutimiza mahitaji yaliyopo.
- Mifumo huundwa na mahitaji, uchakataji, matokeo, mrejesho na mazingira (Daryani, 2012).

Kwa kawaida, mfumo unajulikana kama ni kitu kinachojumuisha vipengele na hatua mbalimbali zinazoingiliana na kutegemeana zenye njia za mrejesho. Kila kipengele na hatua vinahitajika ili kufanya mfumo kamili na wenye kutosheleza wajibu na kazi zake. Katika muktadha wa mfumo wa EUWAWA, vipengele na michakato yote vinavyotakiwa kutoa huduma ya EUWAWA vinazingatiwa. Mfumo unategemea fasili maalumu ya ujifunzaji na elimu ya watu wazima kwa muktadha wa nchi na hugusa sekta na ngazi mbalimbali za utawala. Kujenga mfumo wa EUWAWA ungehusu mchakato wa kupima na kugundua mfumo na kutafuta namna mbadala za kuusanifu/kuuboresha upya, kuujaribu mfumo mpya ulioboreshwa, kufanya marekebisho na kuupanua ili kulifikia kundi la walengwa wengi zaidi.

### Mkabala wa fikira za kimfumo

Fikira za kimfumo ni mkabala wa kusoma kwa makini na kusimamia mifumo tata ya kuleta mrejesho. Kiini cha fikira za kimfumo ni kwamba zinazingatia uhusiano wote ndani na nje ya mfumo ili kuelewa nini kinaendelea, na kutumia maelezo yake ili kuuboresha. Mkabala huu unatambua kwamba sehemu zote za mfumo zinahusiana moja kwa moja au isivyo moja kwa moja. Mara mabadiliko yanapotokea katika sehemu mojawapo yataathiri sehemu zote za mfumo (iwe chanya au hasi).

Mkabala huu unadai mabadiliko ya mara kwa mara na una matokeo na athari juu ya namna taasisi, michakato, ujuzi na watendaji walivyojipanga. Mkabala huu unahitaji ufanyaji kazi na mipaka ya kitaasisi na ngazi za utawala na ushughulikiaji wa matatizo kwa pamoja. Mikabala ya kimfumo inalenga matokeo, inahitaji watendaji mbalimbali ndani na katika ngazi zote za serikali na watendaji wengine kufanya kazi pamoja.

Fikira za kimfumo hutupatia fursa ya kutathimini ugumu wa kazi tunazofanya na kupima namna tunavyoyaangalia matatizo. Hutusaidia kutambua kiini cha matatizo na kuona hatua za kuchukua pale ambapo marekebisho yataleta maana zaidi. Inahusisha kubadilika kimtazamo ili kuona ni kwa namna gani sehemu zote zinahusiana, vilevile kutengeneza zana za kusaidia kuboresha mfumo. Inachukua mtazamo wa muda mrefu wa kutatua matatizo kiuendelevu (CPS HR Consulting).

### Utawala

Dhana ya utawala inaweza kuelezewa kama uwezo wa serikali kutengeneza na kutekeleza sheria, taratibu na kutoa huduma (Fukuyama, 2013). Maana hii inafanana na ile ya Umoja wa Mataifa inayofafanua utawala kama hatua ya kufanya uamuzi, na hatua ya kutekeleza uamuzi (au kutotekeleza). Utawala unaweza kutumika katika mazingira tofautitofauti kwa mfano, utawala wa kampuni, kimataifa, kitaifa na serikali za mitaa.

Hivyo, uchambuzi wa utawala umejikita kwa watendaji rasmi na wasio rasmi ambao hufanya uamuzi na kutekeleza mipango mbalimbali katika ngazi rasmi na zisizo rasmi zilizowekwa kutekeleza

uamuzi. Serikali ni miongoni na ndio mtendaji mkuu wa utawala, na wadau wengine ni asasi zisizo za kiserikali, vyama vya ushirika, taasisi za utafiti na makundi ya kiraia kama vile vyama, n.k.

### Muundo na mchakato

Muundo na mchakato unahusiana na mpangilio wa muundo wa taasisi na vile zilivyopangiliwa kwa mfano mfumo wa utawala, n.k. Pia, inahusisha ushirikiano na uratibu wa ndani kwa mfano kati ya sehemu mbalimbali (Kamati na timu za wafanyakazi) na nje ya mfumo inahusisha sekta mbalimbali za serikali na taasisi za kiraia na wajibu wao.

Hivyo, muundo wa utawala utahusisha ngazi mbalimbali za serikali, wajibu wao na rasilimali, jinsi gani zimepangiliwa, namna yake ya kufanya kazi pamoja na kushirikiana na wadau wengine kubainisha, kutekekeleza na kuboresha sera katika kufanikisha matokeo bora kwa jamii (Eropean Comission, 2017). Muundo wa utawala unaakisi kazi za taasisi au shirika. Kazi za taasisi ni zile zinazohusu matokeo mbalimbali ya kazi za taasisi au shirika hilo kwa mfano bidhaa na huduma ambazo hutolewa.

Michakato husaidia taasisi kufanya kazi. Kuna shughuli mbalimbali zinazohusiana na kila moja ambazo hubadilisha mahitaji (watu, taarifa na fedha, n.k.) kuwa matokeo (huduma zilizotolewa) kufanikisha malengo ya kisera na kiutekelezaji. Mara nyingi, zina changamoto kubwa, hasa kama zinaendeshwa na taasisi zaidi ya moja au hata kazi na vitengo tofauti ndani ya taasisi moja (European Commission, 2017).

### Utoaji wa huduma

Utumishi wa umma (afya, elimu na ustawi wa jamii n.k.) unaweza kueleweka kama ni mwingiliano kati ya serikali na raia, iwe zinatolewa moja kwa moja au kupitia wakala. Kila nchi inapangilia utumishi kutokana na taasisi zake, utamaduni, mahitaji na huhusisha mipaka ya utoaji wa huduma za umma na za binafsi (European Commission, 2017). Ni wazi kwamba serikali peke yake haziwezi kutatua uhitaji unaokua wa huduma za jamii kwa kutekeleza yenyewe tu na zinahitaji kutafuta msaada kutoka katika sekta nyingine za jamii.

Modeli mbalimbali zilizopo na huduma zinaweza kutolewa na serikali moja kwa moja, kupitia ubia kati ya umma na sekta binafsi, au kwa kushirikisha asasi za kiraia, n.k., Ikumbukwe kwamba serikali inabaki kuwa mtoaji huduma bila kujali aina ya utaratibu au mtindo inaoufuata.

Hivyo, EUWAWA ni huduma zinazotolewa kwa vijana na watu wazima kwa mfumo rasmi, usio rasmi au nje ya mfumo rasmi. Inaweza kujumuisha madarasa ya kisomo cha watu wazima, madarasa ya kujifunza

kuinua hali za maisha au mafunzo ya biashara, n.k. Ni lazima yazingatie uhitaji (mahitaji na maslahi ya kundi lengwa) na upande wa 'utoaji huduma,' mipangilio na michakato ya serikali na ushirikiano na wadau katika kutoa huduma.

### Upande wa wahitaji huduma

Upande wa wahitaji wa huduma za umma ni wale wenye haki za msingi. Hii inamaanisha raia mmojammoja na makundi ambayo yana haki na yanahitaji huduma. Maslahi, mahitaji na madai yao ni lazima yachunguzwe na kufahamika katika kupanga na kutekeleza huduma. Vilevile, lazima wawe na fursa ya kuingiliana na watoa huduma na kushauri kuhusu ubora na upatikanaji wa huduma hizo.

### Upande wa watoa huduma

Upande wa watoa huduma unawahusu watekelezaji au vyombo na mashirika yanayowajibika kutoa huduma za umma. Kimsingi, hii ni miundo ya serikali kutoka ngazi ya serikali za mitaa na inajumuisha sekta mbalimbali na ofisi za serikali kama vile elimu, afya, na kilimo n.k. kutegemeana na aina ya huduma. Kama ilivyoandikwa hapo juu, huduma zinaweza kutolewa kupitia wakala wa kati.

### Miradi / Programu

Mara kwa mara huduma hutolewa kwa mtindo wa programu zinazoendeshwa na sekta za serikali, kama vile "Mpango wa Taifa wa Kisomo cha Watu Wazima". Inapotekelezwa na Asasi isiyo ya serikali hujulikana kama mradi hivyo ni muhimu kutofautisha kati ya miradi na programu.

Programu hujikita katika uratibu wa miradi mbalimbali na shughuli nyingine kwa kipindi fulani ili kuleta matokeo fulani. Kwa asili, usimamizi wa programu ni wa kimkakati na huwa na kazi nyingi. Miradi inachukua eneo dogo la kiutekelezaji na inajikita katika kuleta matokeo, viashirio na kazi za jitihada moja. Miradi inaweza kuhusianishwa na mkakati au EUWAWAmpango wa programu. Miradi midogo inayotekelezwa na wadau wasio wa serikali inaweza kutoa ushahidi wa mfano kwa kupanua upeo wa utekelezaji na kushawishi sera za serikali. Matokeo ya mradi yanaweza pia kutumika kuimarisha matokeo ya programu kubwa.

## 6.2 Kutoa fasili ya kimuktadha na wigo wa kutumia mkabala

Ikumbukwe kwamba EUWAWA haiishii kwenye Stadi za Watu Wazima za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) na siyo elimu kwa watu masikini. Bali ni zana ya maendeleo ya binadamu na kujitegemea. Ni jumuishi kwa umri, jinsia, kabila, historia na lazima ichukue vipengele mbalimbali vya maisha ya watu ili kuelewa mahitaji ya kujifunza na kusanifu programu na huduma ambazo zinaweza kutimiza mahitaji hayo (ICAE, 1994).

Inatambulika kwamba nchi mbalimbali kwa kuzingatia mazingira yake hufafanua umri wa mtu mzima na kujikita katika maeneo ya vipaumbele vya programu katika maana pana ya EUWAWA na mafunzo ya maisha. Kwa mfano, Ethiopia ina elimu ya juu, EMAU (Elimu na Mafunzo ya Ufundi) na elimu nje ya mfumo rasmi ya katika muundo wa Elimu Changamani ya Watu Wazima. Katika nchi nyingi, mifumo ya elimu ya juu na ufundi imeendelezwa vizuri, na zaidi ni taasisi na mifumo ambayo inajishughulisha na elimu isiyo rasmi na elimu nje ya mfumo rasmi ambayo inakumbana na changamoto, kama vile ukosefu wa vipaumbele, bajeti finyu kwa sekta ya elimu na ukosefu wa wafanyakazi wenye sifa, n.k.

MKMEUWAWA na Kiunzi cha nadharia ni pana, kinadharia, zinaweza kufaa katika sehemu yoyote ya sekta husika. Vilevile, mkabala unalenga miradi na programu za elimu isiyo rasmi inayojikita katika kisomo cha watu wazima chenye manufaa, ufundi na ujuzi wa kujikimu kama vile kilimo, biashara, stadi za maisha na mfumo mwingine wa mafunzo ambao unaweza kuwa mzuri kwa jamii zao katika mazingira, afya, vijana au wanawake na elimu ya uraia.

Hivyo, kabla ya kutumia MKMEUWAWA hatua ya kwanza ni kwa wadau kutambua eneo la kujikita katika kujenga mfumo ndani ya fikra pana ya EUWAWA. Hii hutegemea uelewa wa nchi na ufafanuzi wa EUWAWA. Kwa upande fulani, hii ina maana finyu kuhusu kisomo cha watu wazima na katika njia nyingine changamani. Kwa hiyo, ni muhimu kuelezea maana, msamiati na vipengele ya programu mahususi, ambazo sekta na watekelezaji watashirikishwa, vilevile sehemu ya umri wa kundi lengwa, n.k.

## 6.3 Wadau na watekeleza wajibu

MKMEUWAWA unawahusu watoa huduma na watumiaji wa mafunzo na elimu ya watu wazima. Kwa kuwa lengo lake kuu ni kuboresha huduma za mafunzo ya watu wazima, watumiaji wakubwa wa mkabala huu wapo katika upande wa watoa huduma kama inavyoainishwa:

- Ofisi za serikali katika ngazi za taifa na serikali za mitaa na sekta zote zinazojishughulisha na masuala ya watu wazima mfano; Sekta za elimu, kilimo, ufundi, jinsia, n.k.).
- Asasi za kiraia zikiwamo mashirika yasiyo ya serikali ya kitaifa na kimataifa.
- Taasisi za elimu kama vile vyuo vikuu na vyuo vya kati.
- Mashirika ya misaada na washirika wa maendeleo.

Kila mdau atawajibika kutokana na mamlaka na wajibu wake ndani ya mfumo. Mkabala unatambua watumiaji wa huduma kwa kutoa tathmini ya watumiaji kupima uhitaji na matamanio ya vijana na watu wazima binafsi au katika vikundi vya kijamii vilivyoratibiwa. Maoni yao katika huduma ya mafunzo ya watu wazima yanapimwa mwanzoni na wakati wa mchakato wa kujenga mfumo ili kuhakikisha kwamba mfumo unabaki kuwa halisi na unatatua mahitaji ya kundi lengwa. Zana za kadi za alama zinajumuishwa kuwezesha wanafunzi kutaja mahitaji yao na ubora wa huduma inayotolewa.

Wajibu wa serikali kutoa huduma ya mafunzo ya watu wazima unapata mashiko kwa kuwa mashirika ya kimataifa na kitaifa hayana rasilimali za kuendesha programu au miradi mikubwa inayoweza kuwafikia wanaohitaji huduma ya mafunzo ya watu wazima. MKMEUWAWA unataka wadau kufikiria wajibuna majukumu kuhusu mafunzo ya watu wazima. Ukweli kwamba mafunzo ya watu wazima ni haki ya binadamu una matokeo katika kutoa huduma. Kwa hiyo, MKMEUWAWA unasisitiza kusaidia serikali kutimiza wajibu

wake kama mtekelezaji katika ngazi zote za utekelezaji. Katika hali hii, wajibu wa mashirika yasiyo ya serikali na wadau wengine wanaweza kuelezewa katika mazingira ya nchi husika. Sehemu ya kwanza ya mkabala inajikita katika kujenga makubaliano kuhusiana na wajibu na majukumu yao.

Mashirika yasiyo ya serikali yanaweza kutekeleza wajibu mbalimbali kama vile kujaza maeneo wazi ya huduma, kuishauri serikali kukubali baadhi ya tofauti katika kutatua matatizo kupitia ushawishi wenye ushahidi, utetezi wa utengenezaji na utekelezaji wa sera, ushiriki katika kurekebisha programu za umma kulingana na maslahi ya kundi lengwa na kushirikiana na maofisa wa serikali na mawakala (Nocoleta, 2019).

MKMEUWAWA unachukulia kwamba mifumo ya Asasi Zisizo za Serikali na serikali inasaidiana. Kwa kuelezea wajibu na majukumu kupitia kujenga mchakato wa kujenga maelewano kila mdau anaweza kuchangia kwa usahihi na jitihada inayotakiwa zaidi, ujuzi na rasilimali za kujenga mafunzo endelevu ya watu wazima. Zana mbalimbali za ushirikiano zinaweza kutumika kutokana na uwezo unaoletwa na kila mdau katika mchakato. Vyuo vikuu vina wajibu kuendeleza utaalamu wa kitaaluma wa watu wazima, utafiti katika masuala mbalimbali ili kushawishi sera na utendaji bora na mengineyo.


Wadau wote wanatakiwa kutathmini wajibu, majukumu, uimara na udhaifu na kupangilia kazi zao na uwezo wa kuendeleza dira ya maendeleo ya taifa ya elimu na mafunzo ya watu wazima. Hivyo, ushirikiano na umiliki wa mchakato huu ni wa msingi katika mafanikio ya kujenga mfumo endelevu.

# 7. KIUNZI DHANA CHA MKMEUWAWA NA AWAMU ZAKE

Katika kiini cha MKMEUWAWA kuna kiunzi cha dhana ambacho huchukua vipengele na vijenzi vya mfumo mzima wa elimu na ujifunzaji wa watu wazima. Kiunzi cha dhana kimewasilishwa hapo chini kikifuatiwa na maelezo ya vipengele na vijenzi vyake (Angalia sehemu ya 7.1). MKMEUWAWA unatekelezwa katika awamu tano, ambazo zinafafanuliwa katika sehemu ya 7.2. Kila sehemu inaelezwa kwa kina katika vitabu vinavyosalia katika Seti ya Zana za MKMEUWAWA.

Kwa kawaida, mfumo unaeleweka kama kitu kinachoundwa na vipengele tofauti, miundo na michakato ambayo inaingiliana na kutegemeana na njia za mrejesho. Kila kipengele na mchakato kinahitajika kukamilisha mfumo kamili na inahitajika kutimiza wajibu na kazi zake. Katika muktadha wa EUWAWA kila kipengele kinachohitajika kufanikisha huduma hizi, lazima kifikiriwe. Inahusisha maana maalumu na eneo la EUWAWA katika mazingira ya nchi. Kujenga mfumo kunajumuisha mchakato wa kutathmini na kupima mfumo na kutafuta njia mbadala za kusanifu tena/kuboresha mfumo, kuujaribu mfumo ulioboreshwa, kufanya marekebisho na kupanua utekelezaji ili kulifikia kundi kubwa la walengwa katika eneo la kijiografia, mfano nchi nzima.

## 7.1 Kiunzi dhana cha MKMEUWAWA




*Rejea: Adult Learning and Education System - Conceptual Framework: (Belete, 2018*

## Kiunzi dhana cha MKMEUWAWA

Kiunzi dhana katika kurasa zilizopita kinapendekeza kwamba mfumo wa EUWAWA unapaswa kuangalia sehemu zote za utawala katika ngazi mbalimbali. Hii hutegemea muundo wa utawala katika nchi husika. Mzunguko wa duara huwasilisha kila sehemu ya utawala na inaashiria kile kiitwacho 'mwingiliano wima' ikimaanisha muunganiko wa maeneo na katika kila ngazi. Kama mawanda na fasili ya EUWAWA zina mwingiliano wa asili, ambao unaangalia huduma kama vile kisomo chenye manufaa kwa watu wazima ukichanganya na mafunzo ya stadi nje ya mfumo rasmi 'mwingilino wa mlalo' huduma hizi za EUWAWA zinaeleweka na kutolewa kwa pamoja katika maeneo ya utawala (ngazi za juu, kati na chini).

## Vipengele na vijenzi vya mfumo

Ili kuwa na mfumo kamili unaofanya kazi kikamilifu, vipengele vinne vifuatavyo vinahitajika, navyo ni:

- **Mazingira wezeshi:** haya yanahusu sera, mikakati, maelekezo na utekelezaji wa miongozo ya programu n.k. Haya huleta mazingira wezeshi kwa utekelezaji wa programu. Ingawa mazingira wezeshi kwa kawaida yanatengenezwa katika ngazi za kitaifa na watekelezaji wa wajibu wa kutengeneza sera, mikakati na miongozo n.k., (Mfano Wizara za kitaifa), vitabu hivi vinapaswa kutafsiriwa katika ngazi za chini za serikali na kutekelezwa katika ngazi za jamii. Hivyo, muunganiko kati ya ngazi hizo ni muhimu kuuendeleza.
- **Mpangilio wa kitaasisi:** Mfumo unaofanya kazi unaonesha kwamba wadau wanawajibika katika ngazi mbalimbali kadiri ya mamlaka yao kuhakikisha huduma za EUWAWA zinatolewa katika jamii (kadiri ya upeo na maana yake katika nchi). Mpangilio wa kitaasisi unamaanisha utaratibu ndani ya taasisi kwa mfano (muundo wa utawala na mipangilio mingine ndani ya taasisi, wafanyakazi, maelekezo ya kazi, vilevile uratibu na mwingiliano wa kazi za kisekta kama vile; vyombo vya uratibu, kamati za kitaalamu zinazojumuisha sekta tofauti ili kupanga, kutekeleza na kufuatilia kwa pamoja. Pia, inajumuisha ubia na asasi za kiraia au asasi zisizo za serikali na wadau wengine nje ya serikali pia wajibu na mchango wanaoweza kuuleta.
- **Michakato ya kitaalamu:** Inahusu kazi ya kiini cha mafunzo ya watu wazima kadiri ya maana yake na mawanda ndani ya mazingira ya nchi husika. Inajumuisha michakato kama vile utengenezaji wa mtaala, utengenezaji wa vitabu/zana na mafunzo kwa wawezeshaji kuhakikisha mafunzo na elimu ya watu wazima vinatolewa.
- **Michakato ya usimamizi:** Inahusu uwezeshaji wa mafunzo ya watu wazima kadiri ya maana yake na mchakato ambapo bila hiyo michakato ya utaalamu haiwezi kuendelea, kwa mfano mipango, bajeti, ufuatiliaji, tathmini na michakato ya uratibu/ushirikiano.



**MUHIMU SANA**

Kumbuka kwamba mistari katika kiunzi dhana kati ya vipengele hivi vinne siyo migumu, inaonesha kwamba michakato inaenda kati ya vipengele vinne vyote kwa uelekeo mlalo na wima. Zaidi, kila kipengele kina umuhimu katika ngazi za utawala na huzingatia maana halisi ya ujifunzaji wa watu wazima na wadau wanaotoa huduma.

Kila kipengele cha mfumo kina vijenzi ambavyo ni lazima viwapo ili mfumo ufanye kazi. Seti ya Zana inaonesha inatoa kipaumbele kwa vijenzi vitano katika kila kipengele, lakini vinaweza kuwa zaidi. Uchaguzi wa vijenzi vitano vya mfumo kwa kila kipengele hufanya mchakato usimamiwe kwa urahisi. Kwa kuwa tunarejelea mfumo ambao una viungo vinavyoingiliana na kutegemeana, ieleweke kwamba vipengele na vijenzi vya mfumo havifanyi kazi peke yake, bali vinaunganishwa kupitia michakato kadhaa. Michakato huwezesha taasisi kufanya kazi. Michakato inajumuisha shughuli mbalimbali zinazoingiliana ambazo hufanya taasisi kugeuza rasilimali (watu, taarifa na fedha n.k.) kuwa mazao (huduma zilizotolewa), ili kufikia malengo ya sera na malengo ya utendaji. Vijenzi katika kila kipengele ni:

| | Vipengele vya Mfumo | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Mazingira Wezeshi** | **Mpangilio wa Kitaasisi** | **Mchakato wa Usimamizi** | **Mchakato wa Kitaalamu** |
| **Vijenzi** | Sera ya EUWAWA | Muundo wa utekelezaji wa EUWAWA | Njia shirikishi za mipango | Mtaala unaozingatia mazingira husika |
| | Mkakati wa EUWAWA | Rasilimali watu | Bajeti toshelevu na ugawaji wa rasilimali | Mpango na njia za EUWAWA |
| | Mwongozo wa utekelezaji wa EUWAWA | Uongozi na menejimenti | Ufuatiliaji na tathmini | Kujenga uwezo wa ngazi zote za utekelezaji |
| | Mfumo wa sifa | Mbinu za uwajibikaji | Mfumo wa TEHAMA | Kuandaa zana za kufundishia |
| | Mfumo wa kisheria | Muundo wa ushirikiano wa serikali na wadau. | Uratibu na mchakato wa ushirikiano | Tathimini ya mwanafunzi |

*Vipengere na vjenzi vyote vimeunganika na vinategemeana na njia za mrejesho.*

**Kumbuka kwamba:**

Vipengele na vijenzi kimsingi vinamaanisha mfumo uliowekwa na serikali kama mtoa huduma mkuu na anawajibika katika huduma za EUWAWA. Msisitizo upo katika mfumo endelevu unaoweza kutoa huduma kwa wajifunzaji ambao ni watu wazima katika taifa, vilevile unaendana na utaratibu ambao unatumika katika mfumo wa afya, au mfumo mzima wa elimu. Inaeleweka kwamba serikali peke yake haiwezi kutimiza wajibu huu. Kama ilivyooelezwa katika kitabu cha Awamu ya Kwanza: Kujenga Makubaliano, aina tofauti za uhusiano wa wadau unaweza kuwapo ambao unashawishi kusanifu na kuendesha EUWAWA katika nchi.

Hivyo, MKMEUWAWA unatambua kwamba miundo, wajibu na majukumu ya wadau tofauti unaweza kuwapo kwa mfano AZISE na watendaji wengine wasio wa serikali wanaweza kutoa huduma kwa niaba ya serikali au kuongezea kwa zile zinazotolewa na serikali. Hatua huchukuliwa kwa vijenzi maalumu ili kutambua wajibu unaofanywa na wadau wasio serikali – tazama Mpangilio wa Kitaasisi na Michakato ya Usimamizi. Mchango wa miradi midogo katika mfumo wa kitaifa unatambulika katika kipande cha kujengea ukiakisi miundo ya ushirikiano (Mipangilio ya Kitaasisi) na iwapo michango hii inatambulika katika ufuatiliaji na tathimini, Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa na wakati wa michakato ya upangaji (tazama maswali ya upimaji ambayo yanajumuisha wajibu wa wadau wasio wa serikali).

Kutokana na matokeo ya kujenga makubaliano katika Awamu ya Kwanza, kila nchi itaelezea tafsiri yake ya kiunzi dhana cha MKMEUWAWA na awamu zake, vipengele na vijenzi katika muktadha wa lengo zima la mkabala – yaani, kujenga mfumo endelevu wa EUWAWA ambao unaweza kutoa huduma kwa wanafunzi katika nchi. Hivyo, wadau wanaohusika na huduma hii watakuwa ni muhimu sana kwa upimaji, ugunduzi na michakato katika awamu zilizobakia, lakini pia kwa kutambua na kuingiza wajibu na mchango wa wadau wengine walio ndani ya mfumo. Uchambuzi na usanifu mbadala (Awamu ya Tatu) unaweza hata kusababisha mpango mpya na miundo ya wadau ili kutoa huduma bora ya EUWAWA nchini.




Vijenzi vya mfumo vimeelezewa kwa mapana hapa chini:

### Mazingira wezeshi

- **Sera** inayoangazia mabadiliko endelevu ya mahitaji ya wanafunzi katika hali ya ushirikishaji na yenye utaratibu wa ufadhili na ubainishaji mzuri wa majukumu ya wadau. MKMEUWAWA unamaanisha sera za umma, una maana ya mfululizo wa mielekeo na uamuzi unaohusiana nayo ambao ulitokana na mazingira na watu kwa muda husika. Kilele chake ni nyaraka rasmi zilizofafanuliwa ikiwa na lengo kwamba serikali inakusudia kujishughulisha na jamii au kikundi cha jamii. Huu ni mfumo mpana wa kiutendaji (Cloete, 2006).

- **Mkakati** unaobeba maana na kuzingatia ujifunzaji na elimu ya watu wazima na kuchangia katika utekelezaji wa sera kwa ngazi zote zinazohusika na utekelezaji. Ni mpangokazi wa kutekeleza Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima kwa muda mrefu ulioelezwa katika sera na mipango muhimu ya maendeleo ya taifa.

- **Kuwapo kwa miongozo ya utekelezaji wa programu ya EUWAWA** kwa wadau wote na watekeleza majukumu kwa kuzingatia maana na programu za EUWAWA. Mwongozo utaelezea mawanda ya EUWAWA, kutenganisha aina za mbinu za EUWAWA (mfano, kisomo chenye manufaa kwa watu wazima, mbinu za maarifa ya usomaji za Freire zilizohuishwa, na mkabala changamani, n.k.), vigezo na viwango vya utekelezaji bora wa programu, hatua za utekelezaji, mfumo na viashirio vya ufuatiliaji na tathmini, n.k. Huu ni waraka wa kiutendaji unaofasili mkakati katika hatua za utekelezaji kwa wadau wote.

- **Mfumo wa kutambua ujuzi na sifa** ambao unaangazia umahiri wa kiwango cha chini, tathimini ya mitaala, ulinganifu, na maelekezo ya uhamishaji wa sifa na ujuzi. Ni chombo kwa ajili ya maendeleo, uainishaji, na utambuzi wa ujuzi, maarifa, kabla ya kujifunza, na umahiri pamoja na hatua endelevu zilizokubaliwa. Ni njia ya kuunda vigezo vilivyopo na vigezo vipya ambavyo ni matokeo ya kujifunza (Bateman na Giles, 2003). Baadhi ya nchi zinaweza zisiwe na mfumo wa kutambua ujuzi na sifa ila zimekuwa zikitumia miongozo ya kitaifa ambayo inaelezea kukubalika kwa ujuzi na sifa (ikijumuisha zinazopatikana kupitia nje ya mfumo rasmi) na njia ya kuendelea kuzifikia fursa za ujifunzaji na elimu.

- **Uwapo wa mfumo wezeshi wa kisheria** kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya elimu na ujifunzaji wa watu wazima. Hii inahusu sheria na miongozo ya kisheria kwa ajili ya utoaji wa huduma za Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima. Kuwapo kwa mifumo ya udhibiti kunaimarisha haki za utoaji huduma za EUWAWA. Baadhi ya nchi zinaweza kuwa na sheria ya elimu inayojumuisha EUWAWA.

### Mipango ya kitaasisi

- **Uwapo wa miundo fanisi ya utekelezaji wa EUWAWA i**nayojumuisha wadau wote. Hii inajumuisha ngazi zote na sekta za kiutawala, kwa mfano, miundo, madaraja, mgawanyo wa kazi na mtiririko wa madaraka. Kwa mfano, hii inamaanisha kuwapo kwa, Kurugenzi ya Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima ndani ya Wizara au Wakala yenye mfumo thabiti katika ngazi za serikali za mitaa. Pia, inaweza kumaanisha mfumo unaojumuisha watoa huduma wasio wa serikali wanaojishughulisha na utoaji wa huduma za EUWAWA kitaifa, kutegemeana na mfumo uliopo katika kila nchi. Zingatia kwamba msisitizo hapa umewekwa katika utoaji wa kiwango kikubwa na endelevu cha huduma za EUWAWA na muundo wa utekelezaji unaoweza kutoa huduma hizo.

- **Uwapo wa rasilimali watu ya kutosha na yenye sifa** ili kutekeleza programu za EUWAWA katika ngazi zote za utekelezaji, hususani ndani ya muundo wa serikali. Rasilimali watu ya EUWAWA itaidhinishwa na chombo rasmi katika jamii kama vile: Utumishi wa Umma kwa kuonesha majukumu, viwango vya mshahara na taratibu kuhusu sifa na uzoefu. Hii pia itahusisha watoa huduma wasio wa serikali ambao wanafanya kazi hiyo kwa niaba ya serikali au kwa kuisadia serikali.

- **Uongozi na usimamizi** wenye kutoa maagizo, mamlaka na maelekezo ya utekelezaji wa EUWAWA. Kimsingi, hii inaihusu serikali, lakini pia inahusisha watoa huduma wengine ambao wana wajibu wa kutoa huduma za EUWAWA kwa kiwango cha juu.

- **Mbinu na taratibu za uwajibikaji zinazohusiana na ugawaji** wa majukumu na ufuatiliaji wa shughuli zilizokamilika kulingana na matokeo yaliyotarajiwa. Hii inahusisha miongozo ya utoaji taarifa, na miundo yake, n.k. Uwajibikaji unahusu kubeba majukumu ya kiutendaji na matokeo, na kuchukua hatua iwapo shughuli husika haijakamilika kwa viwango vilivyotarajiwa. Pia, uwajibikaji ni muhimu ndani ya ushirikiano wa kujenga mfumo. Hii inaweza kufanikiwa kupitia majukumu na wajibu bayana na kufuatilia kufikiwa kwa hatua muhimu, malengo na matarajio yaliyowekwa kwa muda husika.

- **Uwapo wa ushirikiano madhubuti na miundo ya kimtandao** kati ya serikali na watoa huduma mbalimbali wasio wa serikali wanaotekeleza na kutoa huduma za EUWAWA. Kipande hiki cha kujenga mfumo hugundua uwapo wa muundo na aina zake huku mchakato wa shughuli/uratibu na ushirikiano unagunduliwa katika kipengele cha Mchakato wa Usimamizi. Kwa mfano, unaweza kuwa na muundo wa Kamati ya AZISE ambazo rasmi hukutana, hutambuliwa na hushauriana na serikali au AZISE za kimataifa zinazofanya kazi kama kundi tendaji la wafadhili, n.k.

**Mchakato wa usimamizi**

- **Mipango ya mara kwa mara kwa namna shirikishi** yenye kutimiza madhumuni na hatua muhimu. Hii inajumuisha mpangomkakati na mpango wa mwaka n.k. Ndani ya muundo wa serikali kwa kuzingatia ofisi za sekta mbalimbali za serikali zinazohusika, kitaifa hadi serikali za mitaa, mitandao na mashirikiano na watendaji wasio wa serikali, mfano, mchakato wa mpangokazi wa pamoja wa wadau wote wa Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Mafunzo na Elimu ya Watu Wazima (MKMEUWAWA).

- **Uwapo wa bajeti toshelevu na mgawanyo wa rasilimali.** Hii inahusu mgawanyo wa bajeti katika sekta mbalimbali, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, na michango mingine inayotoka katika asasi zisizo za serikali, na wafadhili, n.k., itakayodumu kwa muda mrefu, bajeti inayotolewa na serikali ambayo hupewa kipaumbele katika kipande hiki cha mfumo. Inaweza pia kuhusisha ufadhili wa serikali/msaada kwa ajili ya watoa huduma wasio wa serikali kutoa huduma kwa niaba ya serikali.

- **Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini** ambao unakusanya na kuchambua data na taarifa mara kwa mara. Mfumo unatakiwa uwe na viashirio na utofautishe shughuli za ufuatiliaji, fedha, matokeo, kufanya tathmini ya matokeo na taathira zake. Inapaswa iwe na njia mbadala za kukusanya takwimu na taarifa kutoka kwa wadau wote.

- **Mfumo wa usimamizi wa taarifa** unaotunza takwimu na taarifa zilizokusanywa kutokana na ufuatiliaji na tathmini na kuruhusu upatikanaji wa taarifa kwa ajili ya kufuatilia na kuchambua maendeleo ya programu kwa ajili ya utekelezaji wa huduma za EUWAWA.

- **Mchakato wa uratibu na ushirikiano** kwa ajili ya mawasiliano/uratibu wa ndani ya taasisi pamoja na mawasiliano/uratibu nje ya taasisi zenye miundo ya sekta nyinginezo na wadau. Hii inamaanisha aina ya mchakato wa uratibu na ushirikiano. Tofauti zinaweza kufanyika katika vikao vinavyotoa taarifa kwa kila mmoja kuhusu mchakato imara wa kuratibu ambao unaweza kuimarisha uchangamani na ushirikiano, kwa mfano, ushirikiano wa pamoja wa ufuatiliaji na tathmini, kupanga na kuandaa zana.

## Mchakato wa kiufundi

- **Mitaala ya ndani** inayoendana na maslahi na mahitaji ya kundi lengwa la EUWAWA. Zinaweza kufanywa na wafanyakazi wanaofanya shughuli za utekelezaji katika ngazi za chini za serikali ambao wanajua muktadha na taarifa za maslahi na mahitaji ya wajifunzaji. Pia, inazingatia hali ya kimuktadha ya mtaala wa nchi kwa ngazi za chini kama ilivyo katika baadhi ya nchi. Watendaji wasio wa serikali wanaweza kuchangia ufanikishaji katika hatua hii. Inatoa fursa kwa ushirikiano miongoni mwa wabia wa EUWAWA. Msisitizo unawekwa katika mitaala ambayo inaendana na maslahi na mahitaji ya wanafunzi wa EUWAWA na mchakato wa kuendeleza na kuhuisha mitaala/muundo huu.

- **Muundo na mbinu za programu ya EUWAWA** ili kukidhi mahitaji/maslahi ya wajifunzaji. Hii inamaanisha a) vipengele au mawanda mbalimbali ya programu za EUWAWA, kwa mfano, je, programu imechangamana na elimu ya watu wazima, mafunzo ya stadi za maisha n.k? Pia, inamaanisha b) mbinu iliyotumika kuwezesha EUWAWA ni uchangamani kwa wanafunzi (mfano, kisomo chenye manufaa kwa watu wazima, mbinu za maarifa ya usomaji za Freire zilizohuishwa na kisomo cha familia, n.k.). Muundo wa programu utaelekeza aina ya vifaa ambavyo vitatakiwa kuandaliwa, maudhui ya mafunzo ya miongozo ya wawezeshaji, na wanafunzi, n.k.

- **Kukuza uwezo** katika ngazi zote za utekelezaji, kwa mfano, kujumuisha mafunzo ya wakufunzi, wasimamizi, wawezeshaji jamii pamoja na wafanyakazi wanaoshughulika na kupanga, kuandaa bajeti, na ufuatiliaji na tathmini ndani ya mwongozo wa mfumo. Vigezo vya mafunzo havina budi kubainishwa, kwa mfano, kiwango cha chini cha mafunzo kiwe majuma mawili kwa wawezeshaji, n.k. Ama kwa hakika, programu za EUWAWA hazina budi kuwa na mkakati wa kukuza uwezo ambao unahusu weledi wa waelimishaji wote wa watu wazima ndani ya mfumo kuanzia kabla ya kutoa huduma ya mafunzo hadi ngazi za elimu ya juu.




- **Maandalizi ya zana** yanahusu vifaa vyote vinavyohitajika katika kutekeleza programu za EUWAWA, kwa mfano, miongozo ya mafunzo, miongozo ya wawezeshaji, vifaa vya ziada vya usomaji kwa wanafunzi, miongozo ya stadi za biashara, na miongozo ya ufuatiliaji na tathmini, n.k.

- **Upimaji wa wanafunzi** unatakiwa kufanyika mwanzoni na mwishoni mwa programu pamoja na kila robo mwaka au kwa mwaka ili kufuatilia maendeleo ya wanafunzi. Taarifa hizi zinatakiwa kuwekwa vizuri katika kumbumbuku na kuchambuliwa kama sehemu ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Upimaji wa wanafunzi unatakiwa kujikita katika vipengele vyote vya programu ya EUWAWA, kwa mfano, kupima uwezo wa kusoma na kuhesabu, programu ya tathmini na ufuatiliaji wa kisomo (LAMP) na mizani hesabu, miongoni mwa zana zinazoweza kutumika katika sehemu hii.

## 7.2 Awamu za utekelezaji wa mkabala

MKMEUWAWA haujishughulishi na hali ya kutathmini mfumo wa elimu ya watu wazima peke yake bali pia ni mbinu ya muda mrefu yenye lengo la kujenga mfumo endelevu wa elimu ya watu wazima. Kwa kuzingatia hali ya mfumo wakati wa upimaji inaweza kuchukua kuanzia miaka sita hadi 12 au zaidi ili kupata mfumo kamili unaofanya kazi ambao unaweza kutoa huduma za elimu ya watu wazima zinazolengwa na mahitaji. MKMEUWAWA unajumuisha awamu tano kama zinavyoelezwa kwa kifupi hapa chini. Kila awamu inazingatia vipengele vyote na vijenzi vya mfumo kwa mujibu wa kiunzi cha dhana cha MKMEUWAWA katika ngazi zote. Kiunzi hiki nacho huzingatia maana ya programu za EUWAWA na programu nyingine za kisekta. Ingawa awamu hizi hufuatana moja baada ya nyingine, si lazima ziwe katika mfuatano wa aina moja. Kwa mfano, kujenga makubaliano ni mchakato endelevu na tathmini ya hali ya mfumo (Awamu ya Pili) inaweza kurudiwa baada ya kuanza utekelezaji (Awamu ya Nne) ili kujua maendeleo yaliyofikiwa. Mara nyingi wadau wanapenda kujua matokeo ya tathmini (Awamu ya Pili) ili kuelewa udharura wa kujenga mfumo – na kwa hiyo, Awamu ya Pili inaweza kuchangia katika kujenga makubaliano. Maelezo ya kila awamu yamejitosheleza katika mfululizo wa vijitabu vya seti hii ya zana.



### Awamu ya Kwanza: Kujenga makubaliano

Kabla ya kuanza kujenga mchakato wa muda mrefu wa mfumo wa EUWAWA, wadau wote wanatakiwa kukubaliana kwa pamoja kuhusu maslahi, dira na umuhimu wa kuimarisha mfumo wa elimu ya watu wazima kwa kuboresha utoaji wa huduma za elimu ya watu wazima. Wanatakiwa kufikia makubaliano kuhusu mawanda na maana ya mfumo wa EUWAWA utakaoboreshwa na wajibu na kazi za wadau katika mchakato. Awamu hii inaweza kujumuisha hatua za awali za zoezi la kutengeneza dira.

### Awamu ya Pili: Upimaji na utambuzi

Awamu ya pili inajumuisha sehemu mbili.

#### Sehemu ya Kwanza: UPIMAJI

Sehemu ya kwanza ya awamu ya pili inahusisha upimaji wa mfumo uliopo wa EUWAWA. Mchakato huu unaweza kuelezewa kama “vitu muhimu katika mfumo” au kwa maneno mengine, kuzingatia hali na masuala muhimu ya mfumo kulingana na kiunzi cha dhana cha ujenzi wa mfumo. Zana za tathmini hutoa taarifa kwa ajili ya uchambuzi zaidi na taarifa za takwimu katika hali ya zana na alama inayoonesha hali ya mfumo kupitia alama. Hii inaweza kutumika kama takwimu za msingi.

#### Sehemu ya Pili: UTAMBUZI

Mara tu baada ya upimaji kufanyika, changamoto kadhaa zitakuwa zimebainishwa katika vipengele vya mfumo. Hizi changamoto au vikwazo vya kimfumo zinahitaji kuchambuliwa zaidi kwa kutumia zana gunduzi na utafiti ili kujua chanzo cha msingi cha kushindwa kwa mfumo. Hii ni sehemu ya pili ya Awamu ya Pili - utambuzi wa mfumo.

### Awamu ya Tatu: Uchambuzi wa mibadala na usanifu

Mara tu picha halisi ya mfumo inapodhihirika kupitia tafiti za upimaji na utambuzi, wadau wanaweza kuanza kubainisha machaguo mbadala ya kuzuia changamoto, kurahisisha mchakato na kubadili muundo wa utekelezaji, n.k. Machaguo mbadala haya yanatakiwa yalinganishwe na muda unaohitajika katika kuyatekeleza, gharama zinazohusika, na rasilimali zilizopo. Jambo la msingi hapa ni kutafuta njia mbadala na sehemu za kuingilia ambazo zinaweza kuwa na faida zaidi, hii ina maana ya kubainisha sehemu za kuingilia katika mfumo zinazoweza kuleta mabadiliko katika mfumo na kuwa na matokeo chochezi kwa vipengele na vijenzi vingine. Awamu hii itahitimishwa kwa usanifu mpya unaoweza kufanyiwa majaribio katika maeneo yaliyochaguliwa (kwa kuzingatia kiunzi jumuishi cha dhana cha mfumo).

### Awamu ya Nne: Utekelezaji na jaribio

Mfumo mpya uliosanifiwa unaweza kutekelezwa ndani ya miaka mitatu hadi sita ambapo ufanyaji kazi wa mfumo unatakiwa kufuatiliwa kwa karibu na kuweka kumbukumbu. Kwa hiyo, marekebisho ya “papo kwa papo” sharti yafanyike, na yanatakiwa kujaribiwa na kuwekwa katika kumbukumbu pia. Zana za upimaji zilizoelezwa katika awamu ya pili zinaweza kutumika wakati wowote kufuatilia maendeleo na mabadiliko. Inashauriwa kuwa zana kama “mizunguko ya ubora” inayojumuisha wadau wote, itumike mara kwa mara kwa ajili ya utekelezaji na ufanisi wa mfumo mpya uliosanifiwa.

### Awamu ya Tano: Pitia, rekebisha na panua wigo

Mfumo uliojaribiwa sharti ufanyiwe upitiaji mwisho wa mwaka ama miaka mitatu au sita (tena kwa kutumia zana za upimaji kama ilivyoelezwa katika awamu ya Pili) na kulinganisha na takwimu za msingi za upimaji wa kwanza, zilizofanyika katika awamu ya pili. Pia, mabadiliko yatakayofanyika wakati wa majaribio na athari zake sharti zizingatiwe. Mabadiliko ya ziada sharti yafanyike na usanifu wa mwisho sharti ukubaliwe kabla ya kupanua zaidi mfumo wa EUWAWA katika wilaya, mikoa na majimbo mengine au ngazi ya kitaifa. Hii lazima ionekane katika nyaraka rasmi, miongozo na maagizo rasmi, kama toleo rasmi la mfumo wa EUWAWA katika nchi husika. Kwa kuwa mfumo unabadilika na unaingiliana na mazingira ya nje, unapaswa kufuatiliwa wakati wote na kufanya marekebisho muhimu kila baada ya muda. Mifumo yenyewe sio malengo, ila ni njia ya kuboresha utoaji wa huduma.

# 8. MWONGOZO WA KUTUMIA SETI YA ZANA

## 8.1 Muundo wa Seti ya Zana

**Seti ya Zana ya MKMEUWAWA inajumuisha mfululizo wa vijitabu. Vijitabu hivi vinafuatana kimoja baada ya kingine kwa mfuatano sahili na vimepangwa kwa utaratibu ufuatao:**

| Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima: Seti ya Zana za Utekelezaji | |
|---|---|
| **Kijitabu** | **Maudhui** |
| Utangulizi wa mkabala na Seti ya Zana | Kijitabu cha kwanza kinatoa muhtasari wa kina kuhusu mkabala, namna na sababu za kutengeneza, kanuni za msingi, kiunzi cha nadharia, na dhana muhimu. Kinaweka msingi kwa kutambulisha kiunzi kikuu cha nadharia ambacho kinatoa mwongozo wa mkabala ndani ya vipengele, vijenzi na awamu. Ni mwanzo wa vijitabu vinavyofuata. |
| Awamu ya Kwanza: Kujenga Makubaliano | Kijitabu kinaelezea mchakato wa kujenga makubaliano miongoni mwa wadau pamoja na vifaa vya kufanyia kazi ili kutengeneza dira, uchambuzi wa wadau, kielelezo cha ushirikiano, n.k. |
| Awamu ya Pili: Upimaji na ugunduzi<br>Sehemu ya Kwanza: Upimaji<br>Sehemu ya Pili: Ugunduzi | Hiki ni kijitabu kikubwa katika mlolongo wa vijitabu ambacho kinaelezea kwa kina sehemu ya kwanza na ya pili ya Awamu ya Pili. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya mwongozo wa namna ya kufanya tathmini kuhusu hali iliyopo ya mfumo wa EUWAWA kupitia mbinu ya upitiaji katika data taarifa na data takwimu (mbinu alama) katika mfumo. Matokeo na ripoti hizi baadaye huchambuliwa kwa kutumia tafiti gunduzi (Sehemu ya Pili) ili kubaini chanzo cha udhaifu na kushindwa kwa mfumo katika utoaji huduma za EUWAWA. Zana za tathmini kwa pande zote mbili, mtoaji na mhitaji huduma, vimejumuishwa katika kijitabu hiki. |
| Awamu ya Tatu: Uchambuzi wa mibadala na usanifu | Kijitabu hiki kinaelezea namna ya kutumia matokeo ya utafiti yaliyopatikana katika Awamu ya Pili. Kinaelezea mchakato na zana zinazoweza kutumika katika kuchambua matokeo na kufanya uchambuzi mbadala ili kupata sehemu nzuri ya kuanzia ambayo inaweza kuchochea athari katika kuboresha mfumo. Kinaelezea hatua za kusanifu mfumo mpya ambao unaweza kujaribiwa katika awamu ya majaribio. |
| Awamu ya Nne: Utekelezaji na jaribio | Kijitabu hiki kinapendekeza vifaa na mchakato unaotakiwa kufuatwa wakati wa majaribio ya utekelezaji wa mfumo ulioboreshwa. Vifaa hivi hujumuisha ujifunzaji kwa vitendo, na njia ya tathmini binafsi, ubora, n.k. Vifaa hivyo vinasadia katika shughuli za majaribio kukusanya taarifa muhimu kwa ajili ya mafunzo na marekebisho ya Awamu ya Tano. |
| Awamu ya Tano: Pitia, rekebisha na panua wigo | Kijitabu hiki kinaelezea kuhusu zana na namna ya kuzitumia katika majaribio ya upitiaji (tena kwa kutumia zana za upitiaji kutoka Awamu ya Pili zikiunganishwa na zingine), kutoa mapendekezo kwa ajili ya kurekebisha na kuorodhesha mambo ya kuzingatia ili kupanua mfumo ulioboreshwa katika nchi nzima/kitaifa. |

Kila kijitabu kimeelezea maudhui na hatua za mchakato pamoja na zana za majaribio na kisha mafunzo kama mifano. Jukwaa la kidigiti la Shirika la Kimataifa la DVV kwa Afrika linahifadhi taarifa zote kuhusu MKMEUWAWA, ikijumuisha na zana zingine, uwasilishaji wa pawapointi na zana za mafunzo/uwezeshaji.

## 8.2 Kabla ya kutumia mkabala na Seti ya Zana

Asasi na wadau wanaopendelea kutumia mkabala huu wanatakiwa kujadiliana na kufikia makubaliano kuhusu muktadha, upeo, wadau watakaohusika na azma ya kuzingatia mchakato wa kujenga mfumo wa EUWAWA. Asasi yoyote ambayo inapenda kutumia MKMEUWAWA sharti itambue kuwa mkabala huu haulengwi kutumiwa na taasisi moja pekee. Unaangazia mahitaji ya mfumo wa EUWAWA ndani ya nchi na hivyo kuhusisha wadau mbalimbali na wanaotimiza majukumu. Asasi zinaweza kuamua majukumu yatakayotekelezwa kwa kutumia mkabala huu. Asasi yoyote inaweza kuanzisha matumizi ya mkabala huu, wadau wote kwa pamoja ili kujadili pendekezo, na kukubaliana kuanza awamu ya kwanza. Asasi anzilishi inaweza kuanza mchakato kwa kuwaalika wadau teule kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa kwanza, ingawa zoezi la uchambuzi wa wadau katika awamu ya kwanza linatoa fursa ya kubainisha nani atahusika katika mchakato ujao.

MKMEUWAWA ni mkabala wa kina na unahitaji mafunzo na kuyahusisha na maudhui ili yaendane na hali ya nchi husika kabla ya kuanza kutumika. Utekelezaji wa mkabala sharti iwe kazi ya wadau wote na kwa pamoja wamiliki matokeo, mipango na utambuzi wa mafunzo unaosaidia kufanikisha mbinu husika. Kwa hiyo, wadau wote lazima wapate mafunzo katika kila awamu ya mkabala kila baada ya muda na hatimaye kutumia nyenzo na njia za kwao.

Kutumia mkabala kunamaanisha azma ya muda mrefu na wadau wanaweza kusaini mkataba wa makubaliano. Kukamilika kwa awamu zote tano za MKMEUWAWA kunaweza kuchukua miaka sita hadi kumi na mbili, kutegemeana na hali ya nchi husika. Mchakato unahitaji fedha na matumizi ya mkabala yanatakiwa kuwekwa kwenye mapendekezo ya sasa ya ufadhili, bajeti ya serikali na uwezekano wa kuongeza fedha za ziada. Kuhusiana na Bara la Afrika, pendekezo la Shirika la Kimataifa la DVV kwa wafadhili BMZ lilihusu kanuni na awamu za mkabala, ili kupata fedha za kufanya upimaji wa mfumo, n.k. Zingatia kuwa awamu za mkabala sio mpya katika elimu ya watu wazima, na fedha iliyotengwa kwa ajili ya tathmini inaweza kutumika katika kufanya upimaji wa hali ya mfumo. Umakini sharti uwekwe katika kunadi faida za mkabala na umuhimu wa uendelevu wake wa muda mrefu kwa wafadhili na serikali.

Matumizi ya mkabala yanaathiri mtindo wa ufanyaji kazi. Michakato ya mipango na bajeti inatakiwa kuwa na vipengele vya shughuli kwa kila awamu. Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unaweza kuimarishwa kwa kujumuisha vipengele na vijenzi vya mfumo pamoja na zana za alama za taarifa na takwimu. Asasi pia zinaweza kuchagua vipengele vya MKMEUWAWA kutegemeana na hali na mazingira. Maelezo ya shughuli hizi yametolewa kwa mapana katika mfululizo wa vijitabu katika Seti ya Zana.

**Seti ya Zana ya Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (MKMEUWAWA) inatambua na kurejelea istilahi za EUWAWA katika machapisho yafuatayo:**

- Towards an operational definition of Lifelong Learning:
- UIL Working Papers No. 1 (UNICEF Institute for Lifelong Learning, 2015c).
- European Adult Learning Glossary, level2:
- Study on European Terminology in Adult Education for a common language and common understanding and monitoring of the sector. (National Research and Development Centre for Adult Literacy and Numeracy, 2008).
- Terminology of Europen education and training policy:
- A selection of 130 key terms (second edition) (European Centre for the Development of Vocational Training, 2014).

# Marejeleo


Avramovska M., Czerwinski T., Lattke S. (2015).
*Curriculum globALE.*
Bonn, Germany: DVV International and DIE.

Bateman and Giles. (2013).
*Qualifications Frameworks and Quality Assurance of Education and Training.*
New York: World Bank.

Belete, S. (2018).
*Adult Education System Building Approach: Assessment of the current status of the adult education system in Ethiopia – Peer Review Guideline.*
Addis Ababa: DVV International.

Cilliers, W. (n.d.).
An Experiential Learning Process for the Advancement of Previously Disadvantaged Employees in an Industrial Context. In U. o. Pretoria, *Research Methods Chapter 3* (pp. 130 –156). Pretoria: University of Pretoria.

Cloete, W. (2006).
*Improving Public Policy from Theory to Practice.*
Pretoria: Van Schaik Publishers.

CPS HR Consulting. (n.d.).
*Using Systems Thinking to Achieve Results in Organisational Development.*
Retrieved from www.cps.ca.gov.

Daryani, A. (2012).
Organisational Theory, Systems Thinking and System Management.
*International Journal of Organisational Leadership. v.1 (2),* p. 71–79.

Delors, J. (1996).
*Learning: The Treasure Within. Report to UNESCO of the International Commission on Education for the the 21st Century.*
Paris: UNESCO.

Denys, K. (2020).
*Curiculum institutionALE. Framework for Strengthening Institutions of Adult Learningand Education.*
Bonn: DVV International.

Dunbar, M. (2020).
*A Review of Entitlement Systems for LLL. Prepared for UNESCO and ILO, August 2019.*
Geneva: ILO.

DVV International. (2011).
The Adult Education Centre – Education as a Public Responsibility.
*Adult Education and Development, v 71.,* p. 31 – 40.

DVV International. (2014).
Report on the Proceedings of the Adult Education Service Delivery Optimisation Workshop. Uganda Kampala: DVV International.

European Centre for the Development of Vocational Training. (2014).
*Terminology of European education and training policy.*
Luxemburg: Publications Office of the European Union.

European Commission. (2017).
*Quality of Public Administration: A Toolbox for Practitioners.*
Luxemburg: Publications Office of the European Union.

Fukuyama. (2013, January).
What is Governance? *Center for Global Development, Working Paper 314.*

Hinzen, H. (2020).
100 Years of Volkshochschule – 50 Years of DVV International.
In R. Egetenmeyer, *Local and Global Perspective on Adult Education and Lifelong Learning* (pp. 201–213).
Bonn: DVV International.

ICAE. (1994).
Adult Education and Lifelong Learning: Issues, Concerns and Recommendations.
*International Council for Adult Education* (pp. 175 – 184).
Toronto Canada: ICAE.

Lindsey, E. (2006).
*A Rights-Based Approach to Development: An exploration of Cultural Relativism and Universality in Human Rights.*
Massachusetts: Brandeis University.

National Research and Development Centre for Adult Literacy and Numeracy. (2008).
*European Adult Learning Glossary, Level 2.*
London: Institute of Education, University of London.

Nicoleta, C. (2009).
The Role and Importance of Non-Profit Organisation.
*Studies and Scientific Research, Economics Edition no 14,* 14–19.

OECD. (1996).
*Lifelong Learning for All.*
Paris: OECD.

Rogers, A. (2014).
The Base of the Iceberg. Informal Learning and its Impact on Formal and Non-formal Learning. In *Study Guides in Adult Education* (pp. 11–25). Opladen, Berlin, Toronto: Barbara Budrich Publishers.

Schein, E. H. (Vol 1, Number 1).
Kurt Lewin's Change Theory in the Field and in the Classroom: Notes Toward a Model of Managed Learning. *REFLECTIONS.*

Sheng. (n.d.).
*www.unescap.org/pdd.*
Retrieved from United Nations Economic and Social Commission for Asia and Pacific: unescap

UIL. (2010).
*CONFINTEA VI Belem Framework for Action: Harnessing the Power and Potential for Adult Learning and Education for a Viable Future.*
Hamburg: UIL. https://uil.unesco.org/adult-education/confintea/belem-framework-action.

UNESCO. (1990).
*World Declaration on Education for All.*
Paris: UNESCO.

UNESCO. (2000).
*The Dakar Framework for Action: Education for All. Meeting Our Collective Committments.*
New York: UNESCO.

UNESCO. (2015a).
*Education 2030. Incheon Declaration and Framework for Action for the Implementation of Sustainabe Development Goal 4.*
UNESCO.

UNESCO. (2015b).
*Recommendation on Adult Learning and Education.*
Paris: UNESCO.

UNESCO Institute for Lifelong Learning. (2015c).
*Towards an Operational Definition of Lifelong Learning.*
Hamburg: UNESCO.

UNESCO Institute for Lifelong Learning. (2019).
*4th Global Report on Adult Learning and Education.*
Hamburg Germany: UNESCO Institute for Lifelong Learning.

World Bank. (2011).
*Learning for All. Investing in People's Knowledge and Skills to Promote Development.*
Washington: World Bank Group Education Strategy 2020.

DVV International
Mtaa wa Königswinterer 552 b
53227 Bonn
Ujerumani

Simu: +49 (0) 228 97569-0
Nukushi: +49 (0) 228 97569-55
info@dvv-international.de
www.dvv-international.de

## Shirika la DVV International

DVV Internation ni Taasisi ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Deutscher Volkshochschul-Verband e. V. (DVV), Chama cha Elimu ya Watu Wazima cha Ujerumani. Shirika la DVV International linawakilisha maslahi ya vituo vya elimu ya watu wazima (Volkshochschulen) na vyama vyake vya majimbo vipatavyo 900, ambao ni watoaji wakubwa wa elimu nje ya mfumo rasmi nchini Ujerumani. Kama asasi kiongozi na yenye wataalamu katika fani ya elimu ya watu wazima na ushirikiano wa kimaendeleo, DVV International limejizatiti kusaidia ujifunzaji bila kikomo kwa zaidi ya miaka 50. Shirika la DVV International hutoa misaada duniani kote kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza miundo na mifumo endelevu ya elimu ya watu wazima kwa vijana na elimu na ujifunzaji wa watu wazima. Ili kufanikisha hili, Shirika la DVV International hushirikiana na asasi za kiraia, serikali na washirika wa kitaaluma katika nchi zaidi ya 30 katika Afrika, Asia, Amerika ya Kusini na Ulaya. Shirika la DVV International hufadhili kazi zake kupitia fedha kutoka Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Shirikisho la Ujerumani (MBZ), Ofisi ya Masuala ya Kigeni ya Shirikisho la Ujerumani, Umoja wa Ulaya pamoja na wafadhili wengine.

Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (MKMEUWAWA) ni zao la Shirika la DVV International ambalo linaweza kusaidia nchi mbalimbali katika kujenga mifumo endelevu ya Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (EUWAWA) ambayo inaweza kutoa huduma mbalimbali kwa vijana na watu wazima. Seti ya Zana za MKMEUWAWA inajumuisha kiunzi cha dhana cha mkabala pamoja na miongozo na zana za utendaji ili kutekeleza mkabala katika awamu tano.

**Seti ya Zana inajumuisha vitabu vifuatavyo:**

1. Utangulizi wa Mkabala na Seti za Zana
2. Awamu ya Kwanza - Kujenga Makubaliano
3. Awamu ya Pili - Tathmini na Utambuzi
4. Awamu ya Tatu - Uchambuzi wa Mibadala na Usanifu
5. Awamu ya Nne - Utekelezaji na Majaribio
6. Awamu ya Tano - Kagua, Rekebisha na Panua Wigo

**Kwa taarifa zaidi tembelea:**

www.mojaafrica.net
www.dvv-international.de/en/ale-toolbox